Msimulizi, 1893[1]

Edited and corrected by
Arvi Hurskainen
Department of World Cultures, Box 59
FIN-00014 University of Helsinki, Finland
arvi.hurskainen@helsinki.fi

Abstract

This is a corrected version of Msimulizi, the first periodical written and printed in Swahili language. The periodical was established to be an information channel between scattered mission station of the Universities' Mission to Central Africa, and also between the supporters of the mission work in Great Britain. The perodical was originally scanned and made available by SOAS (School of Oriental and African Studies, London). Obvious scanning errors were corrected. Also, clear errors in original print text were corrected. However, nonstandard spelling was not corrected, if it was possible to assume that the writer intended to write in the way it was done.

The file follows the original pagination. A page in the original publication is a page in this file. Page numbering is continuous from year to year, and it is printed at the top of the page.

This file contains the text of year 1893.

MSIMULIZI. 1893
Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,
katika "Universities' Mission to Central Africa,"

KIUNGANI.

Bwana Cook alitoka hapa kama Dec. 12, kwenda barra Newala kufundisha huko, kwani alipata habari kwa simu, ikaletwa na Bwana Askofu ya kwamba atoke hapa aende Newala.

---

[1] The text is issued under licence CC BY-NC

Dec. 18, Mwalimu Yohana pamoja na mwalimu Luke na James Mpila wakawasili hapa kutoka Magila, Wakiwa na hali ya afya, illi wakaleta habari za huzuni, ndizo kufariki mwalimu Lawrence Kombo.

Dec. 20, Mwalirdu Basil Mhada akapelekwa, na pamoja naye mwalimu Antonio Misimile, aliyekuwa mgonjwa wa macho kwa siku nyingi amekwenda huko labda atakuwa heri.

Dec. 23, tukacheza nussu siku kwa upelekwa wa Basil, kwani ni desturi yetu kupewa nuss siku mtu wa Chama cha Paolo Mt.

Dec. 24, Juma a mosi mbele ya Uzaliwa ikawa shughuli yetu kupamba tu, na jioni sala kwa shangwi. Assubui tukaamka kama saa kumi unuss, tukaimba "Carols" mpaka saa thenashara. Saa kwanza ndipo ukafanyika Eukaristi, Wengi Wakashariki. Juma a tatu furaha yetu ikawa kucheza papa hapa. Juma a nne, waana chuoni wote tukaitwa Bububu, shambani kwa Mr. Boustead, akatukaribisha sana, tukatazama maajabu ya mitambo iliopo, na matumizi ya nazi, na ginsi sisi tunavyopoteza mali

MSIMULIZI. 689

kwa kutupa makumbi, na vifuu, kwani yee humpunguzia gharama nyingi kwa kutumia badala ya makaa, na makumbi kufanyiza kamba.

Tukashinda kule, hatta mshuko wa alasiri tukashika njia kurejea zetu hapa, na njia yenyewe ikawa ya baharini kwa chombo.

Juma a tano ukawa mkutano hapa. Watoto wote wa Mkunazini na wa Mbweni wakaja hapa, wakashinda mpaka jioni wakaenda zao.

Alhamisi ikawa kuamka kama majira ya saa kumi unuss, shughuli yetu ikawa kufunga mikeka, na kuweka tayari mizigo ya chakula, kwa nini? Tunaongoza macho pande za shamba, kushinda huko. Bassi zilipotimu kama saa edashara unuss tukang'oa. Safari yetu ikawa kama ya watoto aroba u thalathini, na pamoja nasi, Mr. King, na Mr. Grillanders, na Bwana Archdeacon akafuata nyuma juu ya punda. Bassi tukashika njia pande za kusini, pahala paitwapo Hatajwa. Tukawasili kama majira ya saa tatu. Na Hatajwa ni kilima, kina mawe mengi. msitu umesaki sana, na mapango mengi. Lakini kuna paango moja kubwa sana, ndani mna kiza kikuu. Hatta wenyeji wa kule wamelifanyiza mzimu, hatta kuingia hawaingii illa waanavyali waendapo kutoa uvumba, na ubani, na mdalasini, bassi ndani mmejaa vifuu, na mikungu, ndiyo wanamotolea uvumba &c. Hatta sisi tulipokienda kuingia hawakuamini kama tutarudi wote salama, wakathani tutarudi vipofu, ao macho upande, ao kuumia, na tuliporudi salama wakanena kwa kuwa mlikuwa na mzungu, kwani mzungu na huyo mwenyi mzimu wanapatana sana, kwani wote ni mashetani. Na tukawaonyesha nguo zetu zilizotatuka kwa maana ya msitu, wanasema mmepata hasara kidogo kwa kuingia mle pangoni.

MSIMULIZI. 640

Tena kwa mbali kidogo kama mwendo wa nuss saa kuna paango lingine, nalo kubwa ndani maji baridi swafi, hili jina lake Machomvi, huko watoto walikuwa wakienda koga, na wenyeji pia huoga hapa kwani hawaliogopi mno kama lile la kilimani.

Tena tangu hapo, pwani si mbali, kwani bahari imeingia sana ndani, hatta hii Hatajwa imekuwa kama katika rasi, kwani mkono kwa kuume ndio magharibi, upande wa Chukwani, ndiko bahari kuu, na kwa mkono wa kushoto ndiko mashariki, ilikoingia bahari mpaka ndani, na Hatajwa ni kati.

Na sisi tulifikia katika shamba la Bwana Bakari Biu Nur, lakini mwenyewe hatukumkuta, tulimkuta mkadamo wa shamba, na bibiye Bwana Bakari Bin Nur. Kulipopambazuka assubui ya Ijuma, Bwana Archdeacon akapanda punda kuja zake hapa. Sisi tukakaa mpaka mshuko wa alasiri, tukashika njia kuja zetu. Mtg.

CHITANGALI.

Nov. 18, Bwana Padre wetu amepata mtoto mwanamke ndio furaha iliopo hapa; hatta Nov. 30, siku kuu ya Andrea Mtume na Sh. alibatizwa.

Dec. 12 & 13, tuliwatazamia watoto wanaume akili zao za Chuoni (Examination), tena Dec. 14, & 15 tuliwatazamia watoto waanawake.

Dec. 25, Siku kuu ya Kuzaliwa Bwana wetu, furaha kwa killa mtu. Lakini kwa kweli hapa petu haikustawi hatta kidogo, kwa sababu hatuna Kanisa ndio umasikini wetu, kwani naliwaambieni tumeliangusha tunalijenga lingine kubwa zayidi twatumaini litaisha mwezi huu wa January.

MSIMULIZI. 641

Dec. 26, alituwasilia Mwalimu L. Mkwasomba pamoja na watoto wake watano, tukafurahi kumwona.

Dec. 29, mimi na Mwalimu huyu Leonard tukafuatana kwenda Miwa kutembea tukarudi siku ya pili. Kweli nimesahau habari moja, watu wa hapa petu walifunga safari ya tumbako katika mwezi wa November, kwenda kuuza tumbako. Bassi katika safari ile alikuwamo mwanafunzi jina lake Suya, naye huyo alikuwa mtumwa huko karibu na Machemba, kwa Seyid Machemba. Akaonana na bwanawe akachukuliwa utumwani marra ya pili amekwenda kuuzwa Kilwa Kivinje, ndio huzuni yetu. Na mzee Barnaba Nakaam akaandika barua kumwarifu Dachi wa Mgao Lindi, bassi hatuyajui walivyojibizana. Mwezi wa November tukapata habari kama Machemba bin Mchakama analeta vita hapa Mlolela; nasi tukamtazamia lakini wapi asije. Tena huyo Machemba akapata habari kama Che Barnaba Nakaam anamjia na vita yuko Lukulesi, na Mdachi anamjia upande wa pwani na vita, bassi mzee Machemba na watu wake akakimbia msituni wakalala huko kwa siku tano ao sita: halafu walipoona ni habari za uwongo watu wakarudi mjini.

January 2, tukafuatana kwenda Newala tukafika saa saba, tukakuta mashindano ya pili.

Jan. 3, ilikuwa mashindano kwa watoto. Katika (Examination) alioshinda katika darasa ya kwanza ya watoto waume 1 Kalemwaga, 2 Gideon Kawanga, 3 Nasro. Darasa ya pili wa 1 Banali; 2 Kapanda, 3 Malemula. Darasa ya tatu wa kwanza Mkwemba, 2 Manji; darasa ya nne wa kwanza, Kipili, 2 Kasala, 3 Mbela., Katika darasa ya tano 1 Mpandula, 2 Almasi, darasa ya sita 1 Salimu, 2 Atendemele, 3 Mbungala. Katika watoto waanawake darasa ya kwanza 1 Njilolaga 2 Durham Chiwiwi, 3

MSIMULIZI. 642

Ngondelaga. Darasa ya pili wa kwanza Akwalachia, 2 Asalipa, 3 Ajanjeuli, darasaya tatu, 1 Akumbolela, 2 Akulaiti, 3 Dora. Katika darasa ya nne 1 Agnesi Majaliwa, 2 Ambombe. Kanisa letu karibu kwisha tunatumaini litazinduliwa Jan. 25, Kuongoka Paolo Mtume. H. S. M.

NEWALA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Baada ya salaam nakuletea habari zetu za dunia hii ya Newala.

Panapo Dec. 2, saa thenashara za assubui tukasikia bunduki inalia, marra tukasikia sauti ya kulia, nikatoka kanisani kwenda kusikiliza, nikamkuta mwanafunzi mmoja wa kike ameumizwa sana na risasi, imekata kidole kikubwa cha mkono wa kuume, nikarudi kanisani, tulipotoka tukaenda kumpa dawa, sasa hajambo. Na bunduki hii aliumizwa, kwa bahati tu, kwani mtu mmoja alikuwa akitengeneza, ikamponyoka, bassi risasi ikamwumiza yeye. Siku ile ile safari ya Lindi ikarudi pasipo barua.

Dec. 3, tulipata habari kama jumbe mmoja jina lake Mapunda ameuawa na watu wa Chisanga sababu alionwa kuwa mchawi. Lakini jambo moja likatusikitisha, kwani tulisikia kama mtoto wa yule mchawi, asiye na kosa lolote alichukuliwa mfungwa wakamue, tuliposikia tu Padre Hood akatoka hapa kwenda kwa Chisanga kujaribu kumzuia asimwue. Lakini alipofika njiani akasikia kama wamemua akarudi, tukasikitika sana.

Dec. 8, siku kuu ya Kuchukua mimba Maryam, hatukusoma tukapewa kucheza.

Dec. 12, nalikwenda kwa Liumanga kufanya

MSIMULIZI. 643

kazi ya W. C. Porter kwani mwenyewe alichoka kwa uthaifu. Nikarudi hapa Dec. 15,

Dec. 19, nalitazamia mambo ya chuoni watoto wa Maniamba, anakofundisha mwalimu Yona Selenje. darasa ya 1. aliyotokea kwanza Natika, 2 Mumangile, 3 Namkwenya. Darasa ya pili 1 Manyike, 2 Nchechela 3 Mkanawene.

Dec. 20, Nikaenda kuwatazamia watoto wa mwalimu Bikado mpaka alasiri, kwani yeye ana watoto wengi. Bassi katika darasa ya kwanza, l ni Mkamuli sawa na mtoto wa kike jina lake Achiganisya, 2 Matonda. Darasa ya 2, wa kwanza mtoto wa kike jina Akuwanji, wa pili Kamtande, 3 Mwambe, siku ile ile mwalimu Leonard P. aliwatazamia watoto wa kike wa school ya mwalimu Emma Pesa. akatokea kwanza Aida, 2 Akummuwesi 3 Utangia.

Dec 21, tulianza kwa desturi kutazamia School yetu hapa, mpaka 23 tukamaliza. Bassi Darasa ya kwanza aliyetokea kwanza ni Isaya Mwalinjila, wa pili Cherubini M, watau Lesle, Darasa ya pili Mika T, na Reuben F. N. Darasa Darasa ya 3, Gaio Sifana, 2 Marko Kasembe. Darasa ya 4 Stefano Mloozya, 2 Krusostomo Matipa. Darasa ya 5, 1 Kachinga. 2 Mtambarika. Darasa ya sita 1 Njeleka. 2 Ngama. Darasa ya saba, 1 Chibwana, 2 Liwasya. Darasa ya nane, 1 Mwipita, 2 Mklesya. Darasa ya kenda, 1 Mpipila, 2 Masonga.

Dec. 23, tukafanya kazi juma mosi tayari kwa siku yetu ya furaha. Juma mosi tukapamba Kanisa letu vizuri sana.

Dec. 25, ndipo siku yetu ya furaha kuu. Usharika Mt. Saa ya 1 watu wengi sana wakashariki hatta ikawa kazi kubwa kwa Padre mmoja. Saa 4 zikawa sala za assubui na Ubatizo wa watu 18.

MSIMULIZI. 644

Watoto wa nyumbani 11 na watu wazima 7. Juma atatu watoto wangine na Mwalimu Leonard Mk. wakaenda Chitangali, watoto wangine Masasi. Juma atano wakawasili watoto 17 wa Masasi pamoja na Mwalimu wao N. Kusi, kwani tuliwaita kwa mashindano ya mpira.

Dec. 18, safari yetu ya pwani imerudi na vitu vilivyochelewa kwa Christmas, tukafurahi mno kuziona taa mpya, za mathabahu na msalaba mzuri sana wenyi sanamu ya Bwana wetu juu yake. Lakini ni huzuni kwani hatukupata barua za Unguja hatta moja illa za Ulaya tu.

Alhamisi na juma amosi Bwana Cook aliwafanyizia watu sanamu za taa.

Jan. 1, Siku ya Yohana, watoto wadogo 10 wakabatizwa Jan. 2 Juma atatu, mashindano yetu ya mpira yakaanza. Kati ya watoto wa Masasi na hapa Newala, kwanza ikaonekana vita kali, wallakini Newala kali mno, ikawapiga mabao matatu kwa hapana, ikawa shangwi sana.

Siku ile ile Bwana Cook, na Mwalimu Leonard P. wamekwenda Rovuma, hatta sasa hawajarudi. Jan3, yakawa machezo mengi kwa watoto, mtoto mmoja wa Masasi akawa hodari sana kwa machezo hayo, jina lake Kanjowe. Jan 2, Mwalimu Leonard Mk. Amerudi, kutoka Chitangali pamoja na Mwalimu Hugh. Jan 4, watoto wa kike walio wa Chuoni wamechinjiwa mbuzi wakafanyiwa karamu. Watoto waliokwenda Masasi wamerudi leo. D.M.

MCHEZO WA VITALI.

Siku ya Kuongoka Paolo, tuliazimu kufanya mchezo wa Vitali tukiiga kama ilivyoandikwa katika "Visa ya Kale." Bassi tukawaita watu wengi, watoto wa Mkunazini na Mbwani pia. Sisi wenyewe na watoto wa kazi wa Mkunazini tukakaa darini, tupate kutazama vema chini killa upande, tena kwa chini hapakuwa na nafasi; kwani chini wazungu walikaa juu ya mbao zilizoinuliwa waweze kutazama vema. Bassi mchezo wenyewe ukagawanyika katika sehemu saba, nao ukachezeka hapa uani petu sehemu zote. Ikaanza kama hivi:

SEHEMU YA I.

Bwana Vitali akatokea na rafiki zake wakaja kusimama mbele ya watu, killa mtu amevalia nguo za kitajiri na upindi mkononi. Vitali akawaambia wenziwe wafuatane naye kwenda kuwinda msituni, kwani tuliotesha msitu mkubwa hapa uani. Bassi wakaingia kuwinda killa mtu na mtumwa wake; nyama alikuwa mbuzi, bassi wakasaka nyama wakesha, wakarudi vyao.

Huyu Bwana Vitali alikuwa Arthur Kasembe, na masahibu yake, Luke, Benedict, Lawrence, Cecil, killa mtu na mtumwa wake.

SEHEMU YA II.

Kumbe katika kule kusaka nyama Bwana Vitali akapotea, akawatafuta wenziwe asiwaone, akaita sana wasimwitikie. Bassi katika kuwatafuta wenziwe akatumbukia

MSIMULIZI. 646

shimoni. Na shimo lenyewe lilikuwa lile birika letu kubwa la uani. Hatimaye masahibu yake wakatokea wakamtafuta wasimwone, wakaita sana, asiitikie. Bassi na wao wakashika njia zao.

SEHEMU YA III.

Masikini Masachio akatoka mwenyi shoka begani akienda kuchanja kuni pale msituni, alao apate pesa mbili, tatu, asitirike kidogo. Bwana Vitali akasikia mshindo wa kule kukata kwa Massachio, akaita, na Massachio akaenda kusikiliza, kumbe asikia sauti ya bin Adamu yatoka shimoni. Akisema "Tafathali nitoe humu shimoni kwani nimekaa kwa siku tatu pasipo chakula wala maji." Bassi Massachio akaenda kukata tawi la mti, kumbe amwona nyani anatokea, Massachio akaogopa sana, akataka kwenda zake, lakini yule Vitali akamwita akaja, akatia tawi la pili amwona simba anatokea, Massachio akaanguka kwa hofu, akashika safari. Lakini yule Vitali akadumu kuita, akanena nitakupa mali mengi sana kwani mimi ni tajiri wa Venezia. Bassi Massachio akarudi tena, kwani alisikia akinena nitakupa mali, akarudi apate mali ya kuolea, kumbe akatokea kenge tena. Bassi Massachio akakata tamaa tena. Lakini Vitali akamwahidia, uyumba yake na mali yote yaliyomo. Bassi Massachio akarudi akatia tawi akamwona mtu anatokea, kutoka tu akaanguka chini, kwani njaa imemshika hatta fahamu hana. Bassi Massachio akamletea mkate na maji, akala, akanywa maji, akapata fahamu. Bassi Massachio akamwamsha wakaagana killa mtu akashika njia yake.

Massachio alikuwa Klement Kathibeni, na nyani alikuwa Filipo Segesela, simba alikuwa Elvani Kachawa, na kenge alikuwa Austini Shukuruni.

SEHEMU YA IV.

Maskini Massachio akashika njia kwenda Venezia

MSIMULIZI. 647
jumbani kwa Bwana Vitali, kutwaa jumba na mali yote. Jumba la Vitali lilikuwa juu ya dari la kuni linalokabili Studies za kwanza. Akamkuta Bwana Vitali amebarizi na rafiki zake, wanakunywa kahawa, na kupeana habari zao walivyokwenda siku ile katika kuwinda kwao. Massachio akauliza watumwa kama bwana yumo, nao wakamwambia yumo, jee! watakani? akanena nimekuja kutwaa jumba hili na mali yote kwani nalimwokoa alipokuwa shimoni, watumwa wakaenda kumwarifu Bwana wao haya, akawaambia mtoeni simjui mimi. Watumwa wakamfukuza Massachio kwa kumsukuma na maneno mengi. Masachio akaenda vyake.

SEHEMU YA V.

Maskini Massachio aliposhika njia kwenda nyumbani kwake, kuwasili kwake anakuta nyani, simba, na kenge, Massachio akashikwa na mshangao, hatta hakuweza kutanabahi neno, akawa kama mti, amesimama tu. Marra akaona nyani kama anamwita, akatoka kumfuata, kumbe akakuta kuni zimejaa tele upenumi. Marra bwana simba naye akaenda kumwonyesha mbuzi, na kenge akamtolea jiwe kinwani pake, linang'aa sana Massachio alipoliona akajawa na furaha sana.

Nyumba ya Massachio ilikuwa karibu na mlango wa jikoni.

SEHEMU YA VI.

Akafunga safari kwenda kuuza lile jiwe lake. Bassi maduka yalichaga pale sermala na madalali wakawapo tele, na askari wakitembea huko na huko, wameingia killa mtu katika suruwali na coat, na madalali walivalia methili ya waarabu koko vile, kilemba cha nguo nyeupe na vijoho vyao vya almaria, samawi, na nyekundu. Bassi Massachio akalitia katika mnada lile jiwe lake, madalali wote wakamwona mpuuzi kwani fetha aliokuwa akitaja haipatani na lile jiwe. Bassi alipofika kwa dalali

shimoni. Na shimo lenyewe lilikuwa lile birika letu kubwa la uani. Hatimaye masahibu yake wakatokea wakamtafuta wasimwone, wakaita sana, asiitikie. Bassi na wao wakashika njia zao.

SEHEMU YA VII.

Masikini Masachio akatoka mwenyi shoka begani akienda kuchanja kuni pale msituni, alao apate pesa mbili, tatu, asitirike kidogo. Bwana Vitali akasikia mshindo wa kule kukata kwa Massachio, akaita, na Massachio akaenda kusikiliza, kumbe asikia sauti ya bin Adamu yatoka shimoni. Akisema "Tafathali nitoe humu shimoni kwani nimekaa kwa siku tatu pasipo chakula wala maji." Bassi Massachio akaenda kukata tawi la mti, kumbe amwona nyani anatokea, Massachio akaogopa sana, akataka kwenda zake, lakini yule Vitali akamwita akaja, akatia tawi la pili amwona simba anatokea, Massachio akaanguka kwa hofu, akashika safari. Lakini yule Vitali akadumu kuita, akanena nitakupa mali mengi sana kwani mimi ni tajiri wa Venezia. Bassi Massachio akarudi tena, kwani alisikia akinena nitakupa mali, akarudi apate mali ya kuolea, kumbe akatokea kenge tena. Bassi Massachio akakata tamaa tena. Lakini Vitali akamwahidia, nyumba yake na mali yote yaliyomo. Bassi Massachio akarudi akatia tawi akamwona mtu anatokea, kutoka tu akaanguka chini, kwani njaa imemshika hatta fahamu hana. Bassi Massachio akamletea mkate na maji, akala, akanywa maji, akapata fahamu. Bassi Massachio akamwamsha wakaagana killa mtu akashika njia yake.

Massachio alikuwa Klement Kathibeni, na nyani alikuwa Filipo Segesela, simba alikuwa Elvani Kachawa, na kenge alikuwa Austini Shukuruni.

SEHEMU YA VIII.

Maskini Massachiio akashika njia kwenda Venezia

MSIMULIZI. 647

jumbani kwa Bwana Vitali, kutwaa jumba na mali yote. Jumba la Vitali lilikuwa juu ya dari la kuni linalokabili Studies za kwanza. Akamkuta Bwana Vitali amebarizi na rafiki zake, wanakunywa kahawa, na kupeana habari zao walivyokwenda siku ile katika kuwinda kwao. Massachio akauliza watumwa kama bwana yumo, nao wakamwambia yumo, jee! watakani? akanena nimekuja kutwaa jumba hili na mali yote kwani nalimwokoa alipokuwa shimoni, watumwa wakaenda kumwarifu Bwana wao haya, akawaambia mtoeni simjui mimi. Watumwa wakamfukuza Massachio kwa kumsukuma na maneno mengi. Massachio akaenda vyake.

SEHEMU YA IX.

Maskini Massachio aliposhika njia kwenda nyumbani kwake, kuwasili kwake anakuta nyani, simba, na kenge. Massachio akashikwa na mshangao, hatta hakuweza kutanabahi neno, akawa kama mti, amesimama tu. Marra akaona nyani kama anamwita, akatoka kumfuata, kumbe akakuta kuni zimejaa tele upenuni. Marra bwana simba naye akaenda kumwonyesha mbuzi, na kenge akamtolea jiwe kinwani pake, linang'aa sana Massachio alipoliona akajawa na furaha sana.

Nyumba ya Massachio ilikuwa karibu na mlango wa jikoni.

SEHEMU YA X.

Akafunga safari kwenda kuuza lile jiwe lake. Bassi maduka yalichaga pale sermala na madalali wakawapo tele, na askari wakitembea huko na huko, wameingia killa mtu katika suruwali na coat, na madalali walivalia methili ya waarabu koko vile, kilemba cha nguo nyeupe na vijoho vyao vya almaria, samawi, na nyekundu. Bassi Massachio akalitia katika mnada lile jiwe lake, madalali wote wakamwona mpuuzi kwani fetha aliokuwa akitaja haipatani na lile jiwe. Bassi alipofika kwa dalali

MSIMULIZI. 648
wa mwisho akamwambia "Kem risim," akanena, Bwana nnakuza Rupia mia teen, Bassi dalali akashangaa akamwuza, kama umeiba umeokota hatta uuze hivyo? Massachio akanena nnakuza rupia mia bassi. Dalali akaita askari kuja kumkamata na kumpeleka kwa Sultani, kwani ni mwizi, kwani kama asingeiba asingeuza vile.

SEHEMU YA XI.

Kwanza akatokea mwenyewe Sultani kuja kukaa kitini pake. Naye ameingia mnamo ukanzu, darizi mpaka unyayo, kikoi bungara, kilemba kibun Said, akajitia na utemsi wake, na joho limemshuka tangu mabega mpaka chini. Mavazi yote yakawa kama amezaliwa nayo.

Na wafuasi wake wote wameingia katika urembo na karani amekaa chini yake, na askari huku na huku. Wakamleta Massachio mbele ya Sultani, Sultani akanena mwanzo hatta mwisho, akaeleza akesha, Sultani akanena Bassi wewe ukamwokoa Vitali, naye akakufukuza vibaya mlangoni pake? akanena "Ndio bwana," Haya, kamwite Vitali, marra askari wawili wakaenda kumwita, akaja, Sultani akamweleza habari zote Vitali. Naye akakana kabisa akanena hatta kumjua mimi simjui marra hiyo akatokea nyani, simba, na kenge, kuwa mashahidi wa Massachio. Bassi Sultani akamwonyesha Vitali kama umesema hana shahidi, bassi mashahidi ni hao. Vitali akajaribu kufanya upwaguzi wake wapi isifae neno, bassi akakamatwa akafungwa gerezani, na Massachio akapewa nyumba yake. Huu ndio ukawa mwisho wa machezo. Sehemu hii ikafanyika mwisho wa uani, karibu na chumba cha makasha na chumba cha kulalia watoto.

Sultani alikuwa Mwalimu Yohana, karani wake Kolumba. Mtg.

MSIMULIZI. 649

KIUNGANI.

Jan. 29, Wageni wengi wakaja kutoka Ulaya Ingreza, wakaja pamoja na Mr. Gr. W. Mallender, na kasisi mmoja, anatoka Dorchester, jina lake Mr. Simpson, naye anakaa hapa.

Siku ya Utakaso wa Bikira Maryamu, ulikuwa mchezo wa kuimbato hapa concert wageni wengi wakaja kusikiliza.

Feb. 15 Mr. Kick akasafiri Magila kwenda kutembea tu.

Feb. 22, Mwalimu Peter akaja kutoka Magila, kungojea kuwasili kwa Askofu.

Siku ya Alhamisi March 2, ndipo Askofu akawasili hapa pamoja na Askofu wa Nyasa. Alishuka Mkunazini kama majira ya saa a pili. Arch. akapanda punda kwenda kumkuta kuko huko mjini. Marra Arch. alipofika huko na kuonana na Askofu, akaleta barua ya kwamba tucheze, bassi ikawa kutoka chuoni na kucheza. Hatta zilipotimu kama saa a kenda tukabadili nguo kumngojea Askofu maana alisema atakuja hapa mshuko wa alasiri. Bassi ikawa kumngojea tena, hatta zilipotimu kama saa a kumi tukamwona anakuja, pamoja na Askofu wa Nyasa na wazungu wake wote. Sisi wote tukaenda kumlaki njiani, na kengele zikilia, na bandera inapepea. Ikawa furaha sana kumwona Askofu wetu tena. Lakini hakukaa sana marra akarejea Mkunazini. Nasi tukaambiwa kama tunatakiwa kwenda Mkunazini kusali sala ya jioni huko. Bassi tukala chakula chetu saa athenashara, unuss tukatoka kwenda Mkunasini kusali sala ya jioni kwa shangwi kuu, na kushukuru kwa kuturudia tena Askofu wetu mwenyi afya na nguvu. Tulipokwisha tukarejea zetu hapa tukala, assubuhi tukashika njia tena kwenda Mkunazini kusali sala ya Usharika Mtakatifu. Tuliporeja tena ikawa kucheza mpaka jioni.

MSIMULIZI. 650

Juma a pili ya tatu katika Kwaresima akaja kutia mikono watoto wapata edashara.

Na jioni yake tukaonyeshwa sanamu za taa za mahali pangine pa Inchi takatifu alipopita Bwana Askofu safari hii, na mwenyewe alikuwa akitueleza habari za killa alipopita.

Juma a pili ya nne katika Kwaresima, wote tukashika njia kwenda Mkunazini, na Mbweni pia ikakumba kwenda Mkunazini, kanisa likajaa, wangine wakakaa katika orofa ya Kanisa. Ikawa furaha sana siku hiyo kumwona ndugu yetu Denys Sayite anaingizwa katika daraja ya Ushemasi. Natumaini haikuwa furaha yetu sisi tu lakini ninyi nyote mtakaposikia habari hizi mtakuwa na furaha na shukrani, kwani ni haja yetu wote ilio kuu tunayoomba dayima, "waondokeshwe wangoje watakatifu katika watu weusi," bassi tupatapo haja hiyo hatuna buddi kuwa na shukrani sana. Maaskofu wote wawili walitumia fimbo zao, na Archd. akahubiri. Ikawa sala ya fahari sana siku hiyo, kwa nyimbo na mambo mengi mangine, tukatoka saa atatu. Sasa katika Chama chetu cha Paolo Mtakatifu, ni Kasisi mmoja, na mashemasi watatu, na Wasomaji wanane.

Juma atatu tukacheza kwa ajili ya Mwalimu Denys.

Juma a tano, Maaskofu wote wawili wakaenda Magila, pamoja na Mwalimu Peter Limo, akatiwe daraja yake ya Ushemasi kwenyi jamaa zake, ndio maana hakutiwa hapa pamoja na Mwalimu Denys.

Leo hivi March 20. Bwana Madan anaingia katika mail anakwenda zake Ulaya kupumzika kidogo, wala si kupumzika tu, lakini atakuwa na kazi ya kutazama na kutengeneza vitabu tutakavyotumia sisi sote katika Upelekwa wetu. Mtg.

MSIMULIZI. 651

KOROGWE.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Baada ya salaam, nakuarifu habari za hapa petu.

Jan. 24, alituwasilia hapa ndugu yetu mwalimu John B. Mdoe na mkewe, kuja kukaa hapa mahali pa mwalimu Henry Nasibu, kwani yeye sasa katoka hapa.

Wamasai waliwasili hapa kuvizia, wapate kukamata ng'ombe kwani wana njaa sana kwao siku hizi. Bassi wakaja kujificha katika msitu karibu na mji, wakingojea watu watokee na ng'ombe zao wapate kuwanyang'anya. Bassi mtu mmoja wa mjini akaingia msituni mle, marra akawaona hawa Wamasai, nao wakamwona, yule mtu akajaribu kukimbia lakini wapi wakamfukuza, wakamkamata wakamwua. Bassi marra tena watu wote waliokuwa mashambani wakafukuzwa, mashamba yote yamejaa kelele, wakamwua mwanamke mmoja tena, na wawili wakajeruhi, mmoja ni mke wa Senjoya, jumbe wa hapa. Na yule aliyeuawa ni mwanawe, hatta na jumbe mwenyewe kapona kwa nasibu, kwani alifukuzwa sana, hatta huyu mkewe alipojeruhi ni katika kukimbia, naye hatujui kama atapona.

Feb. 3, Akawasili hapa Dr. Henriques na Andrea K. Mngazija, na fundi W. Taisiri, na Yohana Mwaimu, na wapagazi kumi: huyu Daktari amekuja kukaa hapa pamoja na huyu Andrea K. Mngazija, mpishi.

Feb. 9, Mwalimu John Mdoe akaenda kwa Zigi pamoja na watoto watano. Hatta walipofika mlima wa kwa Mbumbuli wakaona walimofukuzwa Wamasai na askari wa Dachi.

Feb. 10, ametuwasilia hapa Mdachi mmoja jina lake H. Shapartel, na mpishi wake ni ndugu yetu Peter Selenge.

Feb. ll, tukasikia kishindo kikubwa upande wa Zavuza. Bassi watu wa Korogwe wakajifunga bunduki zao. Na

MSIMULIZI. 653
siku ileile assubui twalienda Mkunazini kumwona mwalimu Denys akipokea daraja la Shemasi.

March 14, watu kumi na nne walitiwa mikono na Askofu wetu, watoto nane, wazima sita, na majina ya watoto ni haya: Alfreda Henzerani, Kate Kalembela, Filicita Bungalo, Dorothy Yudith Nyanzala, Hermina Madukio, Mary Edna Abizaye, Laura Masilamu, Lucia Sakumseka. H.S.

NANYANGA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Baada ya salaam nakuarifu ya kwamba habari zetu ni njema, na ile taabu tuliyokuwa nayo sasa imekwisha, kwani mto wetu hapa sasa umejaa tena. Na baba W.C. Porter kanena kama atatuletea bomba lipate kutufaa wakati wa kiangazi. Dec. 17, nalifunga safari Kwenda Masasi kuwa tayari kwa siku kuu ya Kuzaliwa.

Nikapitia kwetu Newala, pamoja na watoto wangu watano, wawili nikawaacha Newala, na watatu nikaenda nao Masasi. Nalifuatana na msomaji Daudi, yeye nikamwacha kwa Akundonde afundishapo Rikado akitazamia watoto, tena tukiendelea mbele kidogo tukamkuta Filipo Chakale anajenga nyumba kwa Akumkaga apate kufundisha hapo.

Tulipofika Chiwambo ikawa kama majira ya saa sita, tukakaa tupate kupika, na hapa ndipo wanapokunywa maji watu wa Chisanga. Bassi wakaja wanaake wateke maji, na walipotusikia sauti zetu wakathani ni vita, wakaogopa sana, wakataka kurudi. Lakini mmoja akasogea zayidi kusikiliza maneno yetu, tena akauliza nani ninyi? Nasi tukamjibu, Sisi watu wa Newala kwa Sultani Matola Bin Mbusi; Bassi

MSIMULIZI. 654

akawaita wenziwe kuja kuteka maji. Tukafika Masasi Dec. 21, Hatta Dec. 27, nikarejea Newala pamoja na mwalimu Nicholas Kusi pamoja na watoto wake.

Nilipofika Newala marra nikafunga safari tena kwenda pwani ya Mikindani. Nikafuatana na Yona Selenje, anayefundisha kwa Maniamba. Tukauthika mno njiani kwa mvua na umande. Tukawasili Mikindani Jan. 13, Tukafika kwa mhindi jina lake Alarikia, rafikiye mwenyi Matola. Tukakaa hatta alasiri, tukafuatana na huyu Alarikia tukaenda bomani kwa Bwana mkubwa, kununua baruti. Naye Alarikia akamwambia kama hawa watoka kwa mwenyi Matola. Bassi akaniuliza kama wajua kusoma Kiingreza? nikamwambia naam, bassi akanipa barua kusoma, naye akatuonyesha enzi yake, akatuonyesha baruti na killa kitu. Assubuhi sisi tukafunga safari kurudi zetu, lakini Alarikia akatuzuia akanena tungoje kwani akataka kumpelekea mwenyi Matola kanda la tende. Bassi tukatoka Jan. 6, Yona S. tukamwacha njiani kwani alikuwa akimtunza mtoto wake, aliyekuwa na jipu.

Na mbele yetu tukasikia kama kuna vita wanapigana Wamakonde na Wayao wa Chisanga na Msusa, kwani walikuwa wakienda pwani, bassi walipokutana wakaanza kupigana, kwani ni adui; vita ikawa kali sana. Mwana Wakiyao akapigana kama inchi yake, wakauawa Wamakonde saba, na Wayao wakafa watatu.

Lakini kwa sababu wale Wayao si inchi yao wengi wakakamatwa kwani hawakujua kwa kwenda. Bassi hapo alipo Mmakonde anatetemeka, kwani anathani Wayao watakuja kuwapiga tena. Lakini Sultani Matola anajaribu kuwapatanisha hawa Wamakonde na wa watu Chisanga. Hatta wale watu waliokamatwa

MSIMULIZI. 655

Matola akaenda kwa Wamakonde hawa kuwatwaa, na kumrundishia mwenyewe Chisanga. Furaha sana hapa petu siku hizi, kwani mji huu wamejaa Waislamu wengi wakubwa kwa wadogo, bassi ni vigumu kuwapata waje wasikilize maneno yetu, lakini siku hizi wanakuja kusikiliza wakubwa kwa wadogo. B.M.

MKUNAZINI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu habari za pande hizi za dunia, ndiyo hizi. Panapo mwezi Jany. 29, sisi huku tulifikiwa na Wageni, wakitoka pande za Ulaya Ingereza. Wenyeji ni hawa: bwana Mallender wa Kiungani na bwana Allen; wageni, ni padre Simpson na Mr. Grinrod, (shemasi); mabwana, Russell, Bradshaw, H. Faulkner; na mabibi, Miss Garrett, na Miss Basham.

Ukitazama katika Msimulizi wa 27, ukurasa 623 utaona kama tulikwenda Mbweni kukaa, kwa sababu ya chuo chetu. Bassi panapo Feby. 6, tulirejea kwetu mjini, kwani chuo chetu kimeisha tengenezwa. Wallakini hatukuingia marra moja kuitumia, kwani vidaka vya vitabu vilikuwa bado kutiwa, bassi ikawa siku mbili, tatu hatuna buddi kusomea barazani hapa. Wallakini baada ya juma tukaingia chuoni mwetu, sasa swafi kwa upande wake. Panapo Feby. 9, alituwasilia Jones mumo wa Lydia Sikujua, karudi toka barra ya Uganda, baada ya miaka mitatu.

Tena mwezi huo huo, karani wetu, Mr Davenport, akaenda Magila kutembea, kaisha kuturudia vile vile. Lakini safari yao ilikuwa ya hatari majira ya kurudi huku Unguja kwani Chombo chao karibu kuzama.

Panapo Feby. 19, nalipata barua kwa C. W. Rehani

MSIMULIZI. 656

aliyesafiri na Askofu Tucker, ya kuwa wamefika Usoga, bado siku tatu tu wataingia Buganda. Barua iliandikwa Dec. 17, 1892. Lakini amepata hasara kidogo ndio vitu vyake vimeibiwa na mtwana mmoja, akauza kwa Wasoga.

Panapo Feby. 21, ndio tumepata huzuni, kwani mke wa Charles A. J. Masegwe amefariki dunia, ugonjwa wa siku chache tu; R.I.P.

Habari nyingine, ndio panapo March 2, pamefika safari ya bwana Askofu wetu, pamoja na Askofu mwingine aendaye Nyasa, na pamoja na wazungu wangine sita nao pia waenda Nyasa. Bassi panapo Ijumaa Feby. 3, usiku, palikuwa na shangwi sawa sawa humu Kanisani, ya nini? ya kushukuru kwa Bwana, kwani Askofu wetu amerudi salama kwetu tena. Mwajua tena kwa siku nyingi tumeomba kwa Bwana tupate Askofu mwingine, bassi sasa tumempata, je tuache kumshukuru Muungu aliyetupa? haiwezekani, ni sharti. Bassi Shangwi ilikuwa siku hiyo, Ah, hainenekani, kwani Christ Church, lilijaa fuchi kwa watu tangu juu hatta chini; na waimbaji ni wale wale wa Kiungani walikuja wote, Bassi Sala ya siku hiyo ilikuwa kubwa. Na maaskofu yote wawili walivalia mavazi yao ya shangwi, bassi ilikuwa fahari sana.

Na hatta siku ya juma apili yake pia palikuwa na shangwi yake. Ilikuwa vizuri sana sana kuangalia shangwi hiyo, maimbaji yalikuwa bara bara.

Feby. 5, usiku killa mtu amejikalia nyumbani mwake, wangine wanajitembelea tu, huko na huko, marra tukaona watu wanakimbia huko na huko, ghafula hiyo, matarumbeta yanalia, Ee jamaa habari gani? hatta mmoja hakujibu kwa ginsi ya mbio, marra hasikia, mwenyi inchi amefariki, bassi tukawa watu wa kutoka na kwenda sikiliza, ikawa kweli, Sayid Ali amefariki, baada ya ugonjwa

MSIMULIZI. 657

wa siku nyingi. Bassi sasa sikiliza mambo yaliotukia, lakini uniwie rathi bwana Msimulizi kwani labda ntasahau mangine.

Wakati ule matarumbeta yalipokuwa yakilia, na ngoma ya vita ya kiaskari ikilia, kumbe kule kwa bwana, kumekwisha jaa killa namna ya watu, hatta mtoto wa Sayid Barghash, akathubutu kuingia ndani akajimilikisha mwenyewe yeye na rafikize tu.

Wallakini bwana habari zilipofika kwa balyozi na manuarini nazo zilikuwapo mbili tu, H.M.S. Philomel na H. M. S. Blanche, wache matata yawe, (na wakati huu General Hatch ameisha kusanya jeshi lake amewagawia bunduki na panga wote tangu Police hatta Askari, wote akawatawanya katika mji kuvizia.)

Kwani wale Baharia wa Manuarini walikuwa katika kujinyosha, bassi tarumbeta lao lilipolia waliamurishwa kuvaa selaha zao na kushusha mashua na kupakia mizinga. Ee bwana, vyote hivyo, tangu manuarini hatta pwani kwa dakika asharini tu yalifanyika mambo yote, bassi waonaje? si ajabu hiyo? Sikia bassi, hawakushuka tu, lakini askari pamoja na mkuu wao wakaenda kumtwaa balyozi, baharia wakashushwa forthani pamoja na mizinga, bassi marra balyozi alipotokea tu na jeshi lake, jeshi la Mabaharia likaunga, marra wakaingia kwa Sayid, je, wathanije, Ee bwana (nakuambia matata,) kumbe hapana yule mzee wetu wa zamani General Mathews, aliisha wasili lewaje barazani kwa Sayid, akawatwaa Waajjemi; wakuu wa mizinga, akawaambia je mwakaa upande wa nani? Khalid ao Waingreza? wakajibu kwako bwana, bassi akawaamrisha wawe tayari, (mambo haya yalitendeka mbele ya balyozi hajaja kwani Waarabu waliisha kujikusanya kutaka kufanya mambo ya vita, bassi ndio maana General Matthews akafanya akili hizo.) kwa mizinga yao na selaha

MSIMULIZI. 658

zao. Bassi balyozi, na jeshi la wanamaji na askari wa manuarini, pamoja na maofsari wao killa mtu na selaha yake tayari, walipotokea tu barazani kwa bwana pamoja na mizinga yao marra Waarabu wakaanza kufyata mkia, wakaona ni vimoto baba, wasithubutu hatta kunena neno, Balyozi akaenenda mlango wa nyumba ya Sultani, ati akauona umefungwa, nani aliyefunga mlango? bwana Khalid, yuko wapi? yuko juu huko, Akawaambia ungueni mlango, yule Khalid akajifanya kukataa, Ee bwana, marra akanena, usipofungua, dakika hii mlango huu ntauvunjilia mbali, Ah, bwana marra ulifunguliwa, marra balyozi, na keptin wa manuarini, akapanda juu na jeshi lake haba. Akamkuta huyo Sayid Khalid amejikalia kitini, marra waliamrishwa (Marines) askari wa kizungu, "Mtieni mikononi," Ah, bwana pasipo kukawia, alitwaa mikononi, akapelekwa nyumbani kwake pamoja na askari wa kumlinda, akafungwa kwa siku nzima kama mtu fullani, kwa sababu ya jeuri ya kuufunga mlango. Usiku papo kwa papo wakapelekwa watu kumwita Sayid Hamed bin Thwein, Yee huyu alijikalia tu asipotumainia riziki kubwa kama hii, bassi akaletwa mbele ya wakuu wa Kiingreza na Warabu pia walikuwapo. Akaulizwa, mhabari kama je wewe utakubali kutwaa ufalme kwa imara yetu, na utatusikiliza tukuambialo? hatta alipoitikia, Ah, marra ilitangazwa Sayid ni bwana Hamed bin Thwein bin Sultan, marra, matarumbeta yakalia ndipo askari wangine wakaenda zao merikebuni, na jeshi lingine likakaa pale pale kungoja, yote yalitendeka usiku hatta saa tano.

Ee bwana siku hiyo mji ulikuwa kimya kana ni watu kumi waliomo mjini hatta ndege gani akilia ungemsikia sauti yake kwa ukimya uliokuwa siku hiyo.

Kweli mambo haya yalitendeka kwa ajabu sana, nakuambia askari walivyolinda mji vizuri sana, hapana

MSIMULIZI. 659

hatta mtu thaifu aliyepotelewa na kitu chake killa mtu alikaa vile vile, askari walidumu kwa siku tatu mchana na usiku, maduka yalifungwa kwa siku mbili.

Siku ya juma a tatu saa nne za assubui ndipo ilipotwekwa bandera ya bwana Thwein, wache mizinga minene pwani na baharini. Bassi sasa yupo atawala, naona ni mfalme mzuri kwani hapendelei yee, wote sawa kwake, Mwarabu, na Mswahili yee ahukumu haki tu, hivyo ndivyo yalivyokwenda mambo yetu ya huku mjini.

Ah, sasa furaha, kwani Hospital yetu imeisha zinduliwa, na watu natumaini, watakuwa wengi wajao kwa Hospital yetu. Siku hiyo palikuja Mabalyozi wengi na mabaharia pia walikuwapo.

Panapo March 16 Askofu wote wameenda Magila pamoja na Peter Limo na wangine.

March 17, Wazungu sita wale waliokuja na Bwana Askofu Hornby (illa mmoja), wameenda Nyasa, majina yao ni haya, Kasisi J. S. Wimbush, mabwana H.M. Pearson, C. M. Kerr, A. H. Butler, W. Cowey, na Bradshaw. Kasisi mmoja jina lake J. T. H. Beasley, amekwenda zake Ulaya, alikaa hapa siku nane tu, marra akashikwa na homa ya nguvu sana, bassi akawa hana buddi kwenda zake Ulaya; kaenda leo March 20 pamoja na Mr Madan aendaye kupata afya kadri, akitumaini kwa rehema za Muungu kuturejea tena mwaka wa pili wakati kama huu.

Hizi ndizo habari. W.E.K.

MSIMULIZI. 660

Tunapopiga chapa habari hizi, tunasikia kwa sim kwa njia ya Tanga, kama Mwalimu Peter Limo ameisha kutiwa Ushemasi huko Magila, Juma a pili ya tano katika Kwaresima.

MSIMULIZI. 661

MAGILA.

Mtengenezaji wa Msimulizi, salaam, na baada ya salaam habari zetu ni hizi. Feb. 12, watoto wetu 5 wa nyumbani wamepewa misalaba, wanaake 2, majina yao ni haya, Mkaka, Zinga, Hamisi, Nyange, Dudu, Makilua, na Machambo. Feb. 14 tulifurahi kumwona ndugu yetu Antonio Mchancha akitoka Kiungani, alirudi kwa sababu ya babaye, kwani amekufa. Feb. 16 mwalimu Peter Limo alitoka hapa kwenda Unguja kumngoja Bwana Askofu akitoka Uingreza aje naye. Feb. 17 walitufikia hapa Mr. Kick na Mr. Davenport wakitoka Unguja.

Tena, ndugu zangu, nathani mtapenda kusikia swali moja nililopewa na mzee mmoja. Feb. 19 nalienda kufundisha watu wa mji mmoja upande wa magharibi toka hapa; bassi nikaanza habari za kuumbwa ulimwengu &c., halafu yake yule mzee akaniuliza habari ya kutoa kuoa wake wawili, (kwani wanajua kama Wamasihiya wa kweli hawahitaji wake wawili) nami hamjibu ndivyo.

Bassi akasema, kama mimi ninao wake wawili, na killa mke ana mtoto mwanamume, na wale watoto wote wawili wakaenda kukaa Mission wapate kufundishwa, nao wote wakajaliwa kuwa waalimu. Hatta siku moja wakaja kwangu wote, nia yao ni kunifundisha mimi niwe Mmasihiya; nami Umasihiya nautaka, lakini nina wake wawili: bassi nawaulizeni ninyi waanangu mlio waalimu, ni nani hapa atakaye nimwache mamaye aende zake

MSIMULIZI. 662

nipate kuwa Mmasihiya? Na ninyi m watoto wangu, tena juu yote waalimu fikirini atakaye nimwache mamaye.

Bassi ndugu mimi nalilijibu nilivyoweza awali hili. Lakini ni watu wanaotaka kuonywa njia ya Muungu tu zayidi.

Feb. 25 Josephine Juma alipata mtoto mume. Na Feb. 27 Mr. Davenport na Charles J. Mkumbukwa wameenda Unguja.

March 15 huzuni yetu iliyotupata ni hii, yule mtoto wa mwalimu Alfred akafariki, naye alidirikiwa kubatizwa na yeye mwenyewe mwalimu, jioni tukaenda mzika.

March 18 tulifurahiwa sana kuwaona Maaskofu wawili Askofu wetu ua Askofu wa Nyasa; na pamoja nao mwalimu Peter Limo, Mr. Allen na Samwil Mhesa aliyetoka Kiungani. March 19 ndipo tulipata furaha sana, kwa sababu ya kupata limbuko la inchi yetu, atakayeweza kutupa namna njema ya kutaka kutenda kazi ya Bwana mavunoni mwake: ndio ya kuamriwa kwake Peter Limo kuwa Shemasi.

Hatta panapo 21 March, furaha tena ya ndugu zetu 16 waliotiwa mikono; watoto wa nyumbani watatu, wa nje saba, na waanake sita.

March 22 tulifikiwa na habari za huzuni kuu sana, kwani tukasikia kama mke wa mwalimu wetu Martin Furahani amekufa huko Misozwe.

March 23 mwalimu Manfred alitoka hapa na mkewe kwenda kuwatunza watoto wa kike wa yule mke wa mwalimu Martin, kwani alikuwa na watoto wa kike aliowatwaa kukaa nao bassi walikuwa wakingojea kutiwa mikono. March 27 tulionyeshwa sanamu za Mateso ya Bwana wetu kanisani. April 1 tulipamba kanisa letu kama tulivyoweza. Hatta jioni ikawa sala kubwa sana. Tena mwalimu Manfred ndipo aliporudi toka Misozwe.

April 2. ndio siku kuu yenyewe, assubui ikawa Usharika

MSIMULIZI. 665

Mt. na mahubiri, aliyekuwapo ni Bwana Askofu, saa nne ikawa sala ya assubuhi, watu wengi sana walikuja kanisani. Hatta alasiri Askofu wa Nyasa na Mr. Kick walienda Msaraka, tayari kwa safari ya Unguja. Na saa kenda ya usiku Bwana Askofu wetu alitoka hapa kwenda kuwakuta wenzake huko na kushukia njia ya Tanga kwenda Unguja.

Juma tatu April 3 tulipewa sote siku nzima ya kucheza, na watoto nussu walienda kutembea kwao, na watoto 12 walienda Kologwe na Dr. Ley na Mr. Henriques, kwani naye alikuja hapa na watoto, walienda kushindana mpila na watoto wa Kologwe. April 5 watoto waliobaki walienda Msaraka na Mr. Roberts, nao walichukua kondoo na mchele wao, na jioni Alhamisi wakarudi. April 8 tumefurahiwa sana kuwaona ndugu zetu waliotoka Unguja, ndio mwalimu Karlo, Connie Mgoma, Lawrence Mmaka, Edward Kingodi, William Ngoma, Yakobo Chamdangwe. Tena alasiri wale watoto waliokuwa wameenda Kologwe wakarudi, nao wameshinda kwa mpila. April 10 tukaanza Examination ya watoto wetu. April 13 ilikuwa arusi ya mwalimu George Swedi na Jessie binti Ali.

April 16 walitiwa watu 18 kuwa waanafunzi. Waume saba na wake sita, na wale waanaume saba na waanake wawili wanatoka kwa Mkului kwa mwalimu Granville, na wale waanake wanne wanakaa hapa Magila.

Kesho ni April 19 watoto watapata ruksa wa kwenda kukaa kwao. A.A.S.

MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu.
Baada ya salamu nakuarifu kama katika siku kuu ya

MSIMULIZI. 664

Pasaka, twalifurahi sana, watu wengi waliohshariki assubuhi.

Juma tatu, na juma nne, tulicheza tu killa mtu kwake.

April 8. Watoto wadogo walichezesha michezo yao, walikaribishwa Maaskofu wawili, Askofu wetu na Askofu wa Nyasa, na Wazungu wengine wengi wakaja kutazama.

April 14. Twalikaribishwa shambani kwa bibi kwa siku ya kuzaliwa kwake, tukafanyiwa karamu nzuri, tulipewa vitu vitamu alivyotuletea toka Ulaya.

April 25. Siku kuu ya Marko Mtakatifu, wadogo walifanya tena michezo yao, kuwaonyesha wasioona kwanza.

April 30. Alituwasilia bibi mmoja mpya kusayidia nyumba ya kazi, jina lake Miss L. Philips.

May 3. Ilikuwa harusi ya Daudi Kahambwa na Naomi Ngawale, tena ya Martin Zanga na Ruth Agnes Mayufi. Sasa Daudi Kahambwa na Naomi wanakaa Bububu, Martin na Ruth wanakaa Mbweni.

May 11. Siku ya Kupaa ilikuwa furaha sana kwa wote, assubuhi wengi wakaja kanisani, Wamasihiya wengi wakashariki.

Alasiri saa 9 waalimu walikaribishwa na Mrs. Key, kwa chai.

May 20. Mbele ya Pentekote usiku wakabatizwa watoto wanne wa nyumbani, majina yao Prisca Kasina, Gladys Daganua, Eleanor Mary Ashua, Janetta Lilikwao.

May 21 Siku ya Pentekote furaha sana kwa wote; jumaa tatu tulicheza hapa hapa juma nne, tulikwenda Chukwani pamoja na Wazungu saba Mr. Key, na Mr. Allen, Mr. Brough na Mr. Chambers, na Mabibi, Mrs. Key, Miss Garrett na Miss L. Philips, jioni tukarejea kwetu. H.S.

MSIMULIZI. 665

Mnamo siku ile ile jioni Ah! Ndugu zetu wa mbali, na wa karibu, twalipata huzuni kuu, Bibi yetu Miss E. M. Bennett alikuwa hawezi sana sana, tulithani usiku ule atatuacha, lakini sivyo, asubuhi yake akapelekwa Mkunazini, kutunzwa katika nyumba ya wagonjwa, aliugua siku tano tu. May 16. Assubuhi mapema juma nne akalala katika Bwana. Ah, ndugu zetu tuliona huzuni mno, yule bibi yetu aliyetupenda sana amefarakana naswi kwa kitambo. Mwili wake ukaletwa na watoto wa kazi wa Mkunazini hapa Mbweni. Ukawekwa katika Kanisa letu la Yohana Mtakatifu; kwanza mchana ikafanyika Litania kwao waliofariki katika Imani. Ikiwa Bibi huyu alikuwa mtu wa Chama ya Mchungaji Mwema, na ya Watakatifu wote, bassi saa ya kuzikwa kwake tukaimba nyimbo hizi 161 na 148. Saa 11 akazikwa. R. I. P.

MASASI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam sana. Jicho lilipotiwa chongo halioni vema.

Baada ya salaam nakuarifu habari za hapa petu. Siku kuu yetu ya Pasaka tukapamba nyumba, jioni ikawa sala, hatta assubuhi, ikawa sala kuu, watu wengi waliokuja kwa sala.

Ilipokwisha sala, saa sita ikawa karamu kwa Wamasihiya. Mbuzi wawili walichinjwa. Siku ya Juma a tano walimu Nicholas Kusi alikwenda Newala kutembea akashinda siku moja, ya pili akarudi Masasi kwa Juma a pili.

Alhamisi mimi nikaondoka hanenda Ilulu kutembea na

MSIMULIZI. 666

kuangalia hali ya inchi, na ginsi wenyeji wanavyostarehe. Juma a tano Mwalimu Nicholas Kusi alikwenda Masorola kutembea na kutafuta watoto, akaleta watoto 11, saba wanaosoma na wangine wamerudi kwao.

Siku hizi twamtazamia Bwana Askofu.

Mimi nilipokwenda Ilulu nalifuatana na mtu wa huko huko aliyekuja huku kuoa, bassi mimi nilipokuwa nikirejea nalirejea na mtu mwingine, yeye nalimwacha, nikawasili peke yangu, naye akanifuata bassi akaumwa na nyoka Longo akafariki nikaletewa habari tu.

Mtoto mmoja wa Sila naye pia amefariki kwa kuumwa na nyoka. Na tena habari za Masasi, mvua shidda sana, jua tu na baridi kali. Tulifurahi kumwona Mr Faulkner aliyekuja kutembea hapa petu, nathani ataleta habari zayidi za hapa. P. K.

MISOZWE.

Twamhuzunikia sana ndugu yetu, Martin Furahani, afanyaye kazi yake Misozwe, imempendeza Muungu kumletea msiba mkuu kwani amefiwa na mkewe, amelala kwa amani. R. I. P.

Na siku hizi mwalimu Cyprian Lizani na mkewe Maryamu wanasayidia kule kule, bassi watoto wa kike wapo vile vile wakisoma.

MLOLELA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu, Baada ya salamu nakuarifu habari zetu za hapa, unajua kama siku hizi tulikuwa katika kujenga Kanisa letu ya Maryamu Mt. Bikira Bassi nasema limekwisha; tungalimaliza zamani lakini shughuli za kulima mashamba. Safari hii ni kubwa

MSIMULIZI. 667

sana, hatta juma a pili ya Mitende tulikuwa na furaha, pa wili; kwanza sababu Muungu ametujalia kufika mwaka huu, tena furaha ya pili ndio kufungua Kanisa hili. Bassi kengele ilipopigwa Wamasihiya na Waanafunzi walikuja wote wameshikana wawili wawili, na majani ya mitende mikononi mwao wote waume kwa wake, Sala za kulizundua Kanisa zikaanzwa, msalaba umetangulia na ubani, tukalizunguka Kanisa wote pamoja kwa kuimba zaburi 51 tukaingia Kanisani wote, tena Litania, kiisha Sala ya Ushirika Mt. halafu watu wa Miwa 12 wakapokea misalaba, waume waanawake 4.

March 22 Yona na Dabora wakapata mtoto mke, Ah! ndugu zetu furaha ikiisha yafuatana na huzuni. March 28 Padre wetu akambatiza mwanafunzi mmoja aliyeungua kitwa sana, halafu akaanza kusema sema maneno mengi akabatizwa, aliitwa Julius Hamisi, 29 akafariki. Ah! masikini mamaye alikuwa nao wawili tu, Lipugwaga na Julius Hamisi, asubui ndio juma a tano mbele ya Pasaka, asubui akatengenezwa akaletwa kwa Sala ya Usharika Mt. akawekwa Kanisani, watu wengi wakaja kungoja mmoja wawili Kanisani, hatta Sala za maziko watu wakaja 279 waliokuja wote maziko makuu amewekwa katika uwanda wa Kanisa. Tunamshukuru Muungu amempa afya Susani Akuwipu, mamaye Ambrosyo Mitande, kwani aliugua sana. March 23 usiku wakafika Ambrosyo Mitande, na Suya, watu wakapiga vigeregere, furaha kuu sana, hatta kupakaa jifu vitwani, furaha sana sana. Jumaa kuu tuliifikiliwa na Edwin Hereford kutoka Haverevere tayari kwa Pasaka. Alifika aththuuri kamili, marra akaingia pamoja naswi kanisani, tukaanza sala zote; mwajua hapa kama Padre ni mmoja. Bassi, alifanya taratibu yote peke, hatta saa tissa u nuss, Juma a mosi mbele ya Pasaka, assubui tukapamba Kanisa letu. Waamasiya pia wakaja kwa kazi hii ya kupamba, jioni wakabatizwa watoto wachanga, Emma na

MSIMULIZI. 668

Jane. Taa zetu tumeanza kuziwasha, nuru yake kama jua. Juma a pili ndio Pasaka. Ee Bwana furaha kubwa sana tukaingia Kanisani na kuimba, na ubani, Msalaba umetangulia, tukaimba sana, wakashariki watu 47 sababu wangine walikuwa vitandani, halafu tulipotoka Wamasihiya wakapokea nyama na mchele, halafu kengele ya pili tukirudi tena kanisani, watu wengi wengi sana tuliokuwapo kanisani, Padre wetu akahutubu.

Juma a tatu akapita hapa Bwana Padre Hood, akapumzika kidogo, marra akatoka kwenda Lindi kwani alikuwa na haraka ya safari, akafika tena mwalimu Daud akitoka Newala, pamoja naye watoto 6.

April 6 waanafunzi wakapokea nyama na mchele mwingi, jioni ikawa michezo, Mangaka na watu wa Masasi wakacheza ngoma za mchetechete, Juma a nne wakafika hapa watoto wa Masasi, ndipo tena michezo ikawa mingi, watu wengi wengi sana sana kwani hapa petu watu karibu na siku kuu kuenda huwaita marafiki zao kuja kwa siku kuu siku zote kwa hivyo watu wa Haverevere, Wamachemba, Kumitema, Wahuchesanga, Masasi, Miwa, Mchemba. Bassi, siku hii April 4 michezo ikazidi sana, ngoma wanja tatu mchetechete, mangaka, masewe, chakula kingi, sana kwa Wamasihiya waliwakaribisha Wamasihiya wenzi wao majumbani na kuwafanyia chakula kingi furaha hii yote ndiyo furaha ya kufunguliwa kanisa letu hili. Juma tano April 5 akafika Harry Mnubi, akitoka Masasi kaenda pwani Lindi, kwa shughuli zake, akafika pamoja na watu, Wamasihiya.

Kwa siku kuu furaha iliyotupata ya Pasaka hii tangu imeanzwa Chitangali haijawa ndio mwaka huu tu.

Juma a tano tena ngoma usiku kucha. Tena L. Pesa akapita hapa kwenda Lindi, kwa shughuri zake, Alhamisi April 6 karamu kwa Wamasihiya wa Masasi, mpunga kwa

MSIMULIZI. 669

mbuzi, tende, sharbati, wakala hatta ukawashinda, Juma a tatu baada ya Pasaka, bunduki nyingi sana, sana, mji wetu ulijaa wageni.

Wamasihiya na Waanafunzi wamefanya kazi sana juu yote mfalme wetu Barnaba Nakaam ameacha shughuli za kulima, hakulima shamba illa alikuwa katika kujenga tu, kiisha ameleta fetha kununua mabakuli ya maua mazuri sana, tena majamvi yakutandika chini. April 9 watoto wa Masasi wametoka kwenda zao. April 10 watoto wa Newala wamekwenda zao na mwalimu Daud. April 10 Akafika Mr. Cook, ukitoka Newala na watoto wawili kuja kuonyesha sanamu, April 13 akatoka kwenda Newala.

Kua heri tutaonana mwaka huu, somo. H.S.M.

Tena Tumesikia kama ndugu zetu waliotoka Unguja kwenda barra wamefika salama huko Mlolela, ndio Mr. Faulkner na waalimu wawili waendao kushika kazi ya Upelekwa, ndio Samwil na Luke, wamefika kule Mlolela, April 27. Na wamekaribishwa vizuri kama walivyoweza.

Tumeambiwa kama ndani ya kanisa jipya wamebatizwa watu 29, katika Siku kuu ya Kupaa, ilikuwa siku ya furaha sana, watu wengi sana walikusanyika kuangalia ndugu zao, wakiingizwa katika kundi la Kimasihiya.

April 14, amefariki mtoto wa Francis Wemba jina lake Jane Wemba. Tena mtoto wa Hamisi amefariki April 25.

Kunako mwezi wa April alikuja Fisi Msokosela akataka kukamata mbuzi, lakini alinaswa mtegoni akapigwa bunduki akafa.

Tena tumeambiwa kama Askofu amefika salama Mlolela May 6 pamoja na waliosafiri naye, tena wapagazi hakuwakosa aliwakuta tayari huko Lindi, ndiye aliyewabatiza watu hawa waliobatizwa, tena Bwana Askofu alikaribishwa Mlolela kwa shangwi sana, bunduki nyingi

MSIMULIZI. 670
walipiga, na vigelegele ndio salamu yake kwa wanaake.

Tena mwalimu Arthur Kasembe tumesikia kama atakaa huko mahali pa mwalimu Hugh S. Mtoka.

Tena tumesikia kama Padre Cecil atashuka hapa Unguja pamoja na Bwana Askofu kwa mkutano wa Makasisi, mwezi wa June na kurudi tena huko Mlolela.

KOLOGWE.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu habari zetu. Kunako Feb. 21 Dr. Henriques na A. K. Mugazija walikwenda Kwasigi, hatta siku ya 24 Padre Chambers na watoto wote wakamfuata kuko huko Kwasigi, hatta panapo Juma atatu akarudi na watoto wote, akamwacha Padre Chambers na mpishi hatta panapo Alhamisi, ndio March 2 Padre akarudi kupasha habari za huko Kwasigi, mpishi alimpiga mamba mkubwa sana, Ah! si shukurani ya Waluvu kwa sababu ya huyu mamba? tena akampiga fumo mkubwa hatta hapo Kologwe nyama zikaja, Wakarudi March 11.

Juma a mosi wamefika hapa Wadaichi watatu na wapagazi wao, wapata 100, wanakwenda Kilimanjaro. Tena leo hivi umewasili hapa msafara mkubwa unatoka Kilimanjaro na Mazinde wameshuka na mbuzi wengi jumla sita mia na ng'ombe 6, hizo zote wamewanyang'anya Wamasai. Ah! Bwana Wadachi wana nguvu, mmoja tu, na askari 8; huyo Mzungu mpishi wake ndugu yetu Peter Selenge kama unamjua. Panapo March 17, Padre Chambers na mwalimu J. B. Mdoe na watoto wawili, Kiwayo na Mgaya, wakaenda kushuhudia mwalimu Peter Limo akitiwa Ushemasi huko Magila kama Alivyoitwa na Bwana kupokea daraja ya Ungoje. Hatta panapo Mach 22, mwalimu J. B. Mdoe akaturudia Padre akamwacha Magila alikuwa

MSIMULIZI. 671

na homa, hatta panapo March 25 Padre akarudia Juma a mosi. Tena siku ile ile Peter Selenge akapita hapa na Mzungu wake wakitoka pwani, wanakwenda Mazinde tena. Tena siku ile ile anatuasilia hapa Mdachi mmoja anatoka Mpale lakini hawezi mkono na mtoto wake ni yule ndugu yetu Tomoso Lukindo, mtoto wa Mkuzi, kama wamjua lakini tukamkaribisha hapa Mission kwa kumtia dawa na chakula na kulala.

Ah! Bwana Msimulizi, panapo March 26 Juma a pili ya Mitende walikuja Wazigua kanisani wake kwa waume pamoja na watoto wao, jumla yao wapata miteen toka kuanzwa mji huu hawajaja watu kama hawa hatta kidogo.

Tena tumefurahi tumepata wanafunzi 5 wa Mission, wawili Lugula na Kagoda, wa nje watatu, Abdalah na Mwagio na Hamdoma na katika hawa watu wazima, bila ya watoto wa Mission, hawa watatu ndio matunda yetu ya kwanza ya Waluvu.

Na sasa kazi yetu inaendelea na Anjili ya Muungu inaenea kidogo kidogo. Na huko Kwasigi Padre alienda kuhubiria Waluvu Anjili ya Muungu. Wametusikia wawezavyo na waliokuja kusikia mahubiri wapata 200, lakini ni upande mmoja wa mji Kwasigi sio wote, kwani mji mkubwa sana kama Kologwe, na killa nyumba watu 5 ao 6 na wake wao. Na kesho Juma a tano, March 29, Dr. Heariques anakwenda Magila ameitwa na Bwana Askofu kupiga kinanda siku ya Pasaka. J.L.M.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Na baada ya salaamu nakuarifu habari za hapa petu. Panapo March 31 ndio Jumaa kuu sisi Wamasihiya wa hapa twalikuwa kanisani pamoja na wanafunzi tukasikiliza mahubiri.

Kwanza akahubiri mwalimu John B. Mdoe, yale maneno matakatifu aliyoyatoa Bwana msalabani, akahubiri maneno manne, tena Padre akahubiri yale matatu ya mwisho. Na

MSIMULIZI. 672

sisi Wamasihiya wa huku tu watu wanane tu, na wanafunzi kumi na wawili. Na hii ndiyo Jumaa Kuu ya kwanza katika mji huu. Bassi ikiisha huzuni tufanyeje? Ah sisi hatuna buddi kuingia katika furaha sana, killa mtu wa kwetu twaona hana buddi kufurahiwa, ndio siku ya Pasaka. Sisi hapa hatta tukiwa wachache lakini tumefurahi sana. Panapo Apr. 4 wametuasilia hapa watoto wa Magila pamoja na Dr Ley, na Dr. Henriques. Na hawa watoto wa Magila wamekuja kwa mashindano ya mpila. Bassi Apr. 6 saa tatu ndio Alhamisi. Mashindano yetu yakaanza kati ya watoto wetu na watoto wa Magila. Ah! lakini bwana, wenzetu wa Magila wamejifunza siku nyingi lakini sisi tumejifundisha kwa miezi miwili tu; hatta wakiwa mafundi kwa kupigana sisi tumejaribu, wameingiza moja tu bassi.

Panapo Apr 7. wakatuaga wakarudi kwao Magila pamoja na Dr. Ley. Siku ileile wakaja wevi wakaiba mali nyingi sana ya Mhindi tunakaa naye hapa jina lake Dosa. Na hao wevi mda wa siku sita wakagundulikana.

Panapo April 10 mimi, na Katharina Mamkuna na mpagazi wangu, twalishika safari ya kwenda Magila kwa matembezi ya siku kuu, siku ileile watoto wetu pia alipewa ruhusa ya juma tatu. Na mimi pia nalikaa kule tangu jumaa tatu Ap. 10 hatta Ap. 29, lakini nalimchukuwa mwalimu Lawrence Mmaka kufuatana naye kwa matembezi yake. Siku ileile watoto wetu pia wakarudi kwao na kwao. Panapo May 1. Ndio juma a tatu mwalimu John. B. Mdoe, na bibi yake, na mwalimu Lawrence wakaenda zao Magila, naye Mwalimu John aendaye kwa matembezi tu, lakini mkewe atamwacha huko Magila.

Panapo May 17. ametuwasilia hapa Mwalimu Yakobo Chamdangwe akitoka Magila tukafurahiwa sana kumwona,

MSIMULIZI. 673
kwani amekuja kukaa huku pamoja nasi.

Panapo May 9 saa 2 ya usiku ametuwasilia Mdachi jina lake Mr. Oscar Neumann, na askari miteni, na wapagazi mia na arobaini, wanakwenda Uganda, lakini kwanza wapitia Kilimajaro kupiga nyama, kwani ndio kazi yao wanayoendea huko, watafika hatta Victoria Nyanza miaka miwili ao mitatu watakaa huko. Na Mr Neumann amekuja na homa kali sana, kwani mvua nyingi siku hizi na matope mengi na maji mengi sana, hatta walipokuwa wakija hapa karibu na petu pana mto jina lake Lwengelea hawakuvuka kwa ginsi maji yalivyokuwa mengi sana, lakini walivuka kwa mashua ya mpila. Na huyo Mdachi Padre Chambers amemkaribisha atakaa hapa hatta apate hajambo.

Panapo May 20 furaha kuu imetupata, kwani tumepata wawili walioingizwa kataka kundi letu kwa Ubatizo mtakatifu, majina yao Benyamini Herbert Kidungwe, na Charles Mattayo Mgayo. Haya ndiyo matunda ya kwanza katika inchi hii ya Luvu. Salamu Wakatabahu. J.L.M.

MKUNAZINI.

Kwa mtengenezaji wa Msimulizi salamu, I11a wa baada ya salamu nahitaji nikuarifu habari kidogo tu za dunia hii ya Unguja ao mjini. Habari ni hizi panapo March 27 ametuasilia mzee wetu Joseph Chabwela, akitoka Mombasa, kwani alienenda huko kutembea kidogo; sasa yu papa hapa na ni msimamizi mkubwa wa Hospitali yetu.

Habari ingine mwajua wote kama panapo Ap 2 ilikuwa Pasaka, bassi, jamaa, eh, waliofayidi sana naona ni watoto wetu wa hapa wa kazi, kwani sikia panapo juma a tatu nyumba ya kazi (ndio watoto wa Mr. Lister) wote pamoja na mimi (nalikaribishwa tu), walikwenda Chukwani kwa

MSIMULIZI. 674

mashua mbili za makasia, kushinda huko siku nzima; walichukua mbuzi mzima na miwa, na mchele pia, wakafurahi sana, na mabwana waliokwenda nao ndio mzee wetu Dr. Hine, Mr. Lister, Mr. Gallenders wa Kiungani, na Mr. H. Faulkner wa Mkunazini, na bwana King pamoja na mwalimu Samwil Chiponde na Luke Chivoko. Wakatufuata kwa miguu.

Hatta kwa ginsi walivyozidi kufurahiwa sana ndio Seyid Hamedi bin Thwein mwenyewe alikuja kule Chukwani ndani ya gari na askari zake wale wapanda frasi, akatukuta huko, tunajichezea tu, marra alipotuwasilia tukamwamkia pale, naye akatupigia salaam, tena akawaanza akina bwana, Je mbona haingii ndani mkabarizi na wala hamli juu ya meza? Tena, Je madafu mmepata, na killa hitaji pia mmepata,? tukajibu, ndio bwana, walakini akazidi kuhimiza madafu - Ee Hamdani Sariboko, lete madafu upesi kwa akina bwana, Ee bwana wache madafu yamiminike, hatta akina bwana mafundi wa madafu, wasifaulu siku hiyo.

Naye bwana mwenyewe alikuja tembea tu kwa dakika kumi moja hivyo marra akashika njia akaenda zake. Naswi tukajikusanya tukajipakia ndani ya mashua zetu tukaja zetu mjini, tukafika kwetu mjini saa mbili za usiku kamili dakika haikuzidi; ndio habari zetu za Chukwani.

Ap. 4 usiku, palikuwa na karamu ya watoto wa kazi wa Mr. Lister, karamu hiyo ni kwa wema wa mzee wetu Daktari na Mr. Lister wakatoa mali kwa kusudi hilo; watu wakajifurahisha sana.

Siku iliofuata palikuwa na karamu tena kwa wema wa watu wale wale, hii ilikuwa juu ya watoto wote waliotoka mle nyumbani wawezao kupatikana kama akina Norman

MSIMULIZI. 675

Namkachapo, William W. Kamna, John Chiwangar na wangine tena, walikuja wengi wakala wakacheza, wakafurahi, wakaenda zao.

Ap. 9. Bwana Askofu katia mikono watu wanne hapa, panapo sala ya mchana nao ni hawa wanaake Elizabeth, Nelly; wanaume, Daudi Kam'na na Joseph Mabruki, mtoto mmoja aliyekuwa wa Mzungu wa Mombasa. Siku ile ile jioni yake watoto wawili wa Bibi Mills wakabatizwa, majina yao Tito Sudi na Petro Kimaramsele.

Ap. 10 pamepita safari ya watoto wa Nyasa wakitoka Kiungani, wameng'oa nanga siku ya pili yake. Panapo Ap. 12 tumemsafirisha bwana P. E. Faulkner pamoja na waalimu hawa Samwil Chiponde na Lake Chivoko, yee Mr. Faulkner aenda pande za Newala, kuangalia kutembea na kupunga upepo, atarejea punde, lakini hao waalimu ni kwa kazi yao. Siku hiyo hiyo jioni yake palikuwa na karamu ya watoto wa Mr. Lister, hii ilitolewa kwa wema wa bwana Archdeacon wa Kiungani, wakala, wakacheza, wakafurahi.

Panapo Ap. 16 Padre Acland-Hood katuwasilia akitoka Newala.

Panapo Ap. 24 mshuko wa alasiri, pametuasilia watoto thenashara wapya, wakitoka kwa Balyozi, majina yao ni haya, Ukolo, Fereji, Msagala, Songolo, Faraji, Tawene, Mabruki, Sudi, Juma, Andumbo, Heri, Nasibu. Watoto hawa wamepakiwa papa hapa, walikuwa wakipelekwa Pemba na Maskati, wangine wamekaa sana hapa Unguja hatta walimfahamu bibi Mills walipomwona tu.

Panapo Ap. 30, pametuasilia wageni wa Ulaya Ingreza ndio: Miss M. Woodward, nduguye Padre H. Woodward wa Magila, na Miss Philips akaaye Mbweni. Na bwana Smith, aendayo Nyasa, kazi yake sermala, rafikiye sana wa Nyasa, hatta ndicho kilichomleta huku upendo

MSIMULIZI. 676

tu, kati ya yeye na Askofu Hornby, naye si mtu kijana, la, ni mzee labda mtu wa miaka settini na kuzidi, ameacha watoto, na mama yao huko kwao, akimfuata rafiki yake.

Panapo May 1 tumempeleka bwana Askofu manuarini akisafiri kwenda Newala akichukua pamoja naye Padre Simpson na Padre B. Smith, na bwana Hunter, huyu alikuwa akikaa Mombasa kwanza, kaacha kule, kuja kwetu. Naye ajua Kiswahili. Panapo May 4, tumeona huzuni na furaha kwa kuwasafirisha mabibi yetu wawili Miss Mills na Dean-Pitt. Kwa furaha sababu waenda zao kupata hewa na baada ya siku watatujia tena.

May 7, akafika hapa Gvay Feruzi wa Kiungani akitoka Nyasa, siku hiyo hiyo, katuasilia mwalimu Granville na mkewe na mtoto mmoja wa huko pande za Magila, wamekuja kutembea kwa siku chache, kwani watoto wao wa chuoni wanavuna nafaka, bassi kwa kadri ya mwezi ao kupungua watoto shidda kupatikana. May 17. Wameenenda kwao tena kwa kushika kazi yao.

Nimekuarifu kama mwezi Ap. 24 tumepata watoto thenashara, bassi mmoja wao alikuwa hawezi sana, hatta kabatizwa kule Hospitali jina lake William Mabruki, wallakini twatumaini atapata hali yake ya kwanza.

May 22. Baada ya Pentekote bibi yetu Miss Boyd na Padre Grindrod waliwachukua watoto wa chuoni, kwenda kushinda nao Ziwani chini ya miembe na kujifurahisha kwa michezo panapo mshuko wa alasiri wakarejea. Siku ya 24 Padre Mercer katuwasilia akitoka Newala, kaja kukaa hapa, kwani Padre wetu Mr. Lawson aenda Magila;

Siku hiyo hiyo palikuwa na kwata Mnazi mmoja, sababu ya siku ya kuzaliwa Queen Victoria. Ee bwana sikia habari za Kwata hiyo, Baharia pamoja na askari zao, wakashuka General Hatch pamoja na jeshi lake wakashuka, tena pana jeshi jipya la Seyid mwenyewe, likaalo mlangoni

MSIMULIZI. 677

kwake siku zote, zamu kwa zamu, pia nalo likashuka, bassi waona, bwana, sehemu tatu za majeshi mbali mbali, mizinga pia ikashuka mdundo ulikuwapo, wa Magoa na wa bwana, bass, baharia hawakushusha wao: bass wacha utamu uwepo wakati wa kuchezesha panga na bunduki killa sehemu kwa zamu yake, awali wale weupe tena wale wale wa General Hatch, wale wa bwana Seyid hawakuchezeshwa, kwani ndio kwanza waingie, illa walipiga bunduki tu na mdundo mpya wa kumwamkia Seyid, nao sio kwa ngoma, illa filimbi tupu, lakini ni mtamu kwa upande wake. Baada ya hayo wakarejea kwao.

May 25, Padre wetu Mr. Lawson kasafiri Magila peke yake, labda kukaa huko sijui.

Na habari za mwisho ndio, labda mtapenda kusikia kama Stephen Shante, Barnabas Mshindo, Michael Gudula, na Christease Uledi wamerudi, baada safari ya miaka mitatu safari ya Kongo ao Kepi. Ndio habari. W. E. K.

KIUNGANI.

Siku kuu ya Pasaka tulifurahi sana hapa. Katika Sala kuu walioshariki walikuwa 96.

Tena furaha moja juu ya haya, katika siku ile aliingia ndugu yetu Benedict Madalito katika Chama cha Paolo Mt. Sasa jumla yake ndio watu 34.

Tena marra ikiisha Pasaka Padre Denys alichukuliwa na Mr Key huko Dar-es-salaam kuanza kazi yake. Ndipo alipotumwa na Askofu, kwani wameonwa kule zayidi ya watu mia, waliokaa Mbweni zamani, wanalima sasa kule. Mahali penyewe panakwitwa Kichelwe, mwendo wa saa moja toka Dar-es-salaam. Pamoja nao wanakaa

MSIMULIZI. 678

mahuru wangine wa Balyozi, na miji ya Wazaramo ipo karibu. Bassi Padre Denys anaanza kazi kule, na kujenga nyumba pia, kiisha atavuka kuoa.

Tena kama April 12, tuliwasafirisha waalimu Samwil Chiponde na Luke Chivoko, kwenda kushika kazi yao huko Newala.

Ap 22. Tulipata watoto tissia waliopakiwa papahapa kwenda Maskati, wakakamatwa baharini. Wengi siku hizi wamepatikana, sisi hapa tumepata kukaribisha jumla yapata 15, na wanne wao Wamasai.

May 1. Tulimsafirisha Bwana Askofu pande za huko,na pamoja naye wakaenda waalimu Yustino Mkandu na Arthur Kasembe kushika kazi ya ualimu kule, wakafuatana watoto wanne wa Kiyao waliokwenda kutazama jamaa yao kuko huko.

Mwezi huu ametuwasilia Gray Feruzi, akitoka Likoma ameshika kazi yake ya kupiga chapa vile vile; lakini twalisikia anakuja na watoto wa Kinyasa, kumbe hapana; siku yenyewe ya safari walighairi. Twatumaini tutawaona halafu.

Tena siku hizi Martin Zanga na Daudi Kahambwa wameoa, wanashika kazi zao vile vile.

May 11, alisafiri mwalimu Herbert Sehiza Mkuzi kutazama jamaa zake. Siku hizi ametuwasilia mwalimu Archie Semmanyi, amekuja kuzidi kusoma hapa.

MKUNAZINI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu, illi wa baada ya salaamu habari za dunia hii ni haba sana safari hii. Kwani kana ujuavyo hatta ule mwezi hupotelewa njia yake siku moja: nami kathalika leo habari zimekwenda upande mwingine. Lakini haithuru, pokea haya yapatikanayo kwa leo hivi, nayo ni haya. Panapo May 28 Padre Denys kawasili kwake Kiinua Mguu. Munamo siku ya thelathini, pamefika wageni wanne wa Ulaya Ingreza, lakini kuna ujuavyo, tumeisha watawanya kwani Padre De Boulay akaa Kiungani, Padre Carnon karejea Newala. Na hapa wapo wawili ndio padre Tyrwhitt na Padre na Daktari Palmer.

Panapo May, siku ya wahedi wa thelathini, pamefika wageni wakitoka pande za Ushambara, ndio Padre Salfey na Padre Chambers. Naona utafahamu waliojia, kwani wakumbuka kana imepita miaka kenda sasa, ni desturi ya Upelekwa wetu kukusanyika pamoja, mapadre na watu wa kufanya mashauri yapasayo kwa watu wa upelekwa huu, bassi hawa ni awali kuasili, illi kusudi wangojee hapa kwa wangine kuwasili.

Mnamo siku ya tano ya mwezi June, hapa Unguja pamewasili mtoto wa Seyidi wa Masikati, kijana tu, wala si mtoto mkubwa, naye kaja na mwenziwe;

MSIMULIZI. 679

wamekuja kukaa hapa. Ee bwana wacha siku hiyo mizinga ya salamu ichage ikapigwa hatta ikaenda sesna. Na hao vijana wakashushwa pwani, wapo hapa Unguja, killa nyakati watembeapo ni juu ya frasi tu na vitwana mbele na nyuma.

Mwezi huu June, kumekuja katika Hospitali yetu Baniani wa katika mail za Hindi kavunjika mguu sanduku lilipolomoka likaja likamtwanga tu, bass mguu bwana uliteketea tu, pasipo rehema, bassi akachukuliwa hobela hobela hatta hapa, ndipo Daktari huyu mpya akafanya kazi yake, akamkata, akamshona, sasa kapona, kaenda kwao na mguu mmoja maskini.

Panapo June 18 mtoto mmoja wa Mkuzi jina lake Mattayo B. Mwakusega, kutuasilia hapa atafuta kazi, kapata hapa, ndio katika Hospitali yetu. Siku iliofuata wametuasilia Padre Griffin na Padre Peter, wakitoka bara Bonde kwa mkutano. Panapo 21 safari ya bara Newala imefika, Asikofu. Padre Porter. Padre Hainee, Padre Cecil, Mwalimu Daudi Machina, na bwana Faulkner, na Leonard Mkwasomba, pamtoja na watoto wa bara hiyo, waendao Kiungani kusoma.

Nimekuarifu ya kuwa wageni wanakusanyika kwa ajili ya mkutano wa mashauri juu ya upelekwa wetu. Bassi panapo June 30 mkutano wa Synod ulianza katika Christ Church, ukaendelea kwa siku tatu, ndipo ukaisha. Na mashauri yaliotolewa hapo siwezi kuandika, kwani killa mtu atasikia kwa Padre wake. Panapo mwezi huu huu July palikuwa na mdundo mnazi mmoja, wa Admeli wa H. M. S. Raleigh, wanamaji wakashuka na uthia wao, wa General Hatch wakashuka, mabwana wakashuka, bassi wacha mnazi mmoja ifunikwe na umati wa watu wajao kuangalia.

Bassi wacha mdundo unene na hiyo mizinga yao kana kuila siku vile vile.

MSIMULIZI. 680

Ukitazama katika Msimulizi wa 29 utaona majina ya watoto thenashara, bassi hao panapo July 8, walibatizwa, na majina yao ni haya, Ayub Ukolo, Martino Msagala, Dunstan Songolo, Leonardo Faraji, Karlo Sudi, Juma Kabeti, Yohana Aridumbo, Percy Heri, Mikael Nasibu, William Maburuki, huyu aliisha batizwa ugonjwani, illi leo hivi ametiwa alama ya msalaba tu. Augustino Fereji, Siprian Tawene. Panapo July 11 imeonwa vema mwalimu Kate apumzike kidogo kwani ana ugonjwa wa macho, bassi yaniuma sana, hivyo ndio maana hawezi kufundisha, bassi watoto aliokuwa akiwafundisha walio wanaume wanasoma katika chuo cha watoto wa hapa wamekuwa watoto wasomao mchana tu.

Hapa Unguja pamekuja habari ya kuwa Wabarawa wanafanya uthia sana pande hizo za juu, bassi mzee wetu General Mathews na General Hatch wametoka hapa pamoja na askari wapata thelatha mia, kuwanglia hao washenzi, wakifanya kwi tu, watiwe moshi. Admeli Bedford kaacha manwari yake Raleigh, yee mwenyewe kaenda mto Zambezi atapanda hatta mto Ruo na Shire kuangalia kazi ya H. M. S; Harold na Mosquito, haya ataendelea mpaka juu Nyasa na baadaye atarejea tena, manwari yake itamfuata nyuma.

Seyid Thweni alikwenenda Chuwin, kakaa siku kathawakatha kwani apenda shamba kuliko mjini, kwani hewa ya kule yamfaa sana, lakini kwa leo hivi yuko mjini, kule Chuwini kasimika mlingoti mkubwa wa bandera kana huu hapa mjini. Tena kalima uwanda mkubwa wa kuchezea kwata askari zake siku aendapo kule. Tena kuna shabaha zimewekwa, akijizoezea mwenyewe kwa mizinga na bunduki, kupiga shabaha. W.E.K.

MSIMULIZI. 681

CHITANGALI.

Kwa Mtengenezaji Salaamu. Baada ya salaamu nakuarifu habari zetu hapa, furaha yetu imezidi. April 13 watu 22 walitoka kwenda Lindi kumlaki Askofu lakini hawakumkuta. April 21 watu wale wakatuwasilia pamoja Mr. Faulkner na waalimu wawili Samwili Ch. na Luke wakakaa hapa siku tatu. Juma a tatu wakatoka kwenda Newala, April 14 Jane mtoto wa F. Weniba akafariki. Usiku wake tukamwua fisi aliingia katika mtego alipotaka kutoka James akampiga gongo la shingo, marra Marko akapiga bunduki akaanguka, marra twasikia vigeregere nikatoka mimi na mbwa Wangu na watoto kwenda kutazama, ah! ee bwanawe mkubwa sana, marra ngoma ya furaha, assubui wakaja mataifa mengi kutazama tumechoma hapa barazani tuchezapo mpila upande uliosalia akaja mwenziwe akamaliza.

April 15 tuliwauwa manyoka mawili makubwa mmoja urefu wake mikono minne unuss na mmoja mikono minne kamili tumepata furaha sana kwa adui hawa. April 28 watu wakatoka tena kwenda kumlaki Bwana Askofu. May 1, Filipo na Yakobo Mitume watoto waume na wanawake wakapokea ushanga na maleso mengi, vikasha, na vidawati. Walifurahi sana kwa zawadi zao wakiisha kupokea wote, wakasimama pamoja wakapiga makofi, kwani ndio shukrani yao si kwa sababu wamepata vitu hivi, lakini wapatapo siku kuu hupiga makofi siku zote.

May 5 tukaanza kumtazamia Bwana Askofu, hatta May 6 aththuri tukamwona mtu wa Masasi Yona siku mbili akaja kutuambia safari iko kwa Simba, marra watu thelathini wakatoka na uti zao kwenda kumlaki Askofu. Marra twasikia tuu, tuu, tuu, ee bwanawe,

MSIMULIZI. 682

furaha gani? akatoka Padre wetu na mzee Barnaba marra waanawake vigeregere furaha kubwa sana sana kundi la waanawake wanalamba mavumbi jifu kupakaa, marra twamwona Baba mkuu kati ya uwingi wa watu waume kwa wake hatta shida kumwona kwa watu kuwa wengi na moshi wa bunduki, furaha ikazidi barazani hapa, kucheza, kupiga bunduki, hatukumwona siku nyingi. Baba huyu alifika na mabwana watatu na walimu wawili Arthur Kasembe na Yustino Mkandu na watoto wanne. Hatukuthani tutamwona Askofu wetu, furaha ya bunduki siku ile hatta mtu akiwa sikioni pako husikii asemalo.

Bwana Askofu amefurahi kutuona, Juma a pili akafanya Usharika Mt. tumepata rupia 20 na pesa 40, kwa sadaka. Usiku mbele ya Juma a pili akahubiri Askofu juu ya Kanisa letu. Juma a pili akahubiri tena assubui, Juma a tatu makasisi wawili na waalimu wakatoka kwenda Newala, tumekaa na Askofu siku sita. Alhamisi assubui mbele ya Usharika Mt. walibatizwa watu 31, usikie somo usisahau, nitakueleza ginsi ya ubatizo wetu, watu wakawa tayari wamesimama na mashahidi yao.

Kanisa letu likawapokea. Bassi ndugu zangu mwasemaje si furaha hii? Alasiri Askofu akatoka kwenda Miwa akaapo mwalimu C. H. Chitenje. May 9 Mr. Faulkner akafika hapa kutoka Masasi kwani tulisikia kama hawezi bassi tulifurahi kumwona hatta leo yupo hapa. May 15 Padre wetu akatoka kwenda Newala kwani aliitwa na Askofu.

May 15 Mr. Mercer akafika akitoka Newala May 10 akatoka kwenda njia ya Unguja, May 16 Alasiri akatoka Mr. Faulkner kwenda Newala akalalia Miwa, May 18 Alhamisi Padre wetu akatoka Newala akapita kwa Akumkanga akaapo Filipo, mpaka Chisanga, akafika

MSIMULIZI. 683

Miwa usiku May 19, alasiri akafika hapa. Pentekote palikuwa ubatizo wa watoto wanane, waume 4 waanake 4. Silwano Malemla mtoto wa Henry Chande na Kandake. Efaim wa Yusuf Mteta, Mika wa Tito N. Hugh wa Sila, Emy wa Sila, Mary R. wa Bartolomayo, Jane wa Tito, Upendo Chipato mtoto wa School, jumla wote waliobatizwa hapa petu 40. Furaha kuu kwetu ukiisha ubatizo ikawa harusi watu 10 Wamasihiya, watu waliooa zamani katika ushenzi, kiisha wakapokea mbaraka.

Juma a tatu ya Utatu Askofu akifika hapa. Juma a nne May 30 akawatia mikono watu wale, alasiri akatoka akienda njia ya Masasi, Juma a tatu baada ya Pentekote watoto watatu wa Miwa wakapokea misalaba, Kalanje, Bushiri, na Mzukani, May 29 akaja mwalimu Daud kutembea na watoto. June 3 akaenda zake Newala. June 12 Baba Padre atatuacha, kwani ashuka huko Unguja.

Kwa heri somo tutaonana tena karibu. June 9, alituasilia Bwana Askofu akitoka Masasi pamoja na watoto waendao kusoma Unguja. Tena June 10, alisafiri hapa mwalimu Daudi M. akienda Unguja pamoja na Askofu. June 11, ndio furaha kwa kuona ndugu Wamasihiya wakipokea Usharika Mt. marra ya kwanza; tena wamefanywa wasomaji wawili Mwalimu Sipriani H. Chitenje, na Mwalimu Hugh S. Mtoka.

June 12, Bwana Askofu pamoja na Baba Cecil wakitoka hapa wakienenda Unguja. H.S.M

LIKOMA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam.

March 29 walituwasilia ndugu zetu wa Msumba kusudi tuwe pamoja kwa sala zetu za Ijumaa Kuu. Na Mr.

MSIMULIZI. 684

Johnson alikuwa hawezi siku ile. Kwa hivyo Archdeacon Maples alihutubu peke yake. Juma a mosi athuuri tukapamba Kanisa. April 2, saa kwanza kengele zikaanza kupigwa, kwa sala yetu kubwa ya Usharika Mt. panapo saa tatu yalikuwa mahubiri kwa watu watokao mijini. Bwana Johnson aliwahubiria. Saa nne tukaingia kanisani kwa sala zetu za Assubui. Siku ile ilikuwapo Ubatizo wa watu 53.

March 3, stima iling'oa hapa kwenda chini, pamoja na Wamasihiya wote wa kule.

Watu wa kazi walikwenda kwao kutembea illa watoto wa chuoni ndio hawakwenda pahali, walikuwa wakicheza mpira. April 16, watoto 10 wa chuoni walifanywa Wanaafunzi. Nyumba nyingi siku hizi zimejengwa kupita za kwanza. Kanisa lingine mpya linajengwa, kwani school yetu tuliyo kuwa tukisomea zamani limekuwa Kanisa.

Mtu mmoja wa Ulisa alikufa April 25 jina lake Ankwamba watu wanasema mtu huyu anaweza kujigeuza kuwa simba. Naye tangu kufa kwake hatta leo hajajigeuza kuwa simba, naye kazikwa karibu yetu, mahali alipozikwa paitwa pa Mbuzi. April 26, ilikuwa harusi ya Rikado Tomaso Mnyeta, na Kumijani, mwanafunzi, tangu April 23 hatta April 25 bwana Atlay na bwana Pullinger walikuwa hawawezi, bwana Pullinger tu Adiya hajambo, lakini bwana Atlay hatta leo yuko kitandani, twalitumaini atakuwa hajambo. Ah! watu wa ng'ambo wanenaje, siku hizi biashara yetu ya pembe, hatupati fayida nazo tukienda Kunkamanga, kwa sababu hapana za thamani. Pale kwanza walikuwa wakizipata pembe, kwa sababu zile nguo walizokuwa wakiiba hapa zilikuwa zikiwapatia fayida. Kwa hivyo wanataka wamwue mlinzi wa hapa jina lake Marko Chulu, yule aliyemwua mwivi mwaka jana. Kusudi wakiisha kumwua, wapate nafasi

MSIMULIZI. 685
ya kuja kuiba, ndizo habari.

Tangu kutoka mwalimu Yohana Chizumulu kwa ule uthia wao, sasa wanahitaji mwalimu, marra mbili mfalme wao Amkumfa amekuja kumwambia bwana Archdeacon kama wataka mwalimu. Lakini maneno hayo hayajatengenezeka vema, mpaka aje bwana Askofu. A. T. M.

MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Nataraja kukuandikia habari zetu kidogo tu. Panapo June 12, tulikwenda kushinda katika shamba la bibi, tena panapo June 10, ilikuwa kusanyiko la Chama cha Mchungaji kwa waalimu, na sisi tunafurahi sana kwa sababu wanaongezeka sana, siku hiyo hiyo waliingizwa ndugu zetu wawili na majina yao ndio Mrs. Key na Lulu Masuke. Tena panapo June 11, ilikuwa siku kuu ya Barnaba Mt. naswi tulifurahi sana, tukaenda kutembea tukashinda katika shamba la bibi, na jioni tukarejea kwetu. Tena panapo June 24, ilikuwa siku kuu ya Yohana Mbatizaji, tulishinda papa hapa petu, wala hatukuenda mahali.

Tena June 29, ilikuwa siku kuu ya Petro Mt. na hiyo pia hatukuenda mahali. Tena panapo July 5, tunahuzunika sana kwa kuwa bibi Burke aliugua sana, naye imempasa aende Ulaya na tunatumaini atarudi tena akijaliwa.

July 18, ilikuwa harusi hapa petu ya Padre Denys na mwalimu Rebeca, tena ilikuwa kusanyiko, bassi watu wengi wakaja, tangu watoto wa Kiungani hatta Mkunazini, wakashinda hapa, na jioni killa mtu akarejea kwake. Panapo July 7, Padre Key aliingia katika Chama cha Mchungaji Mwema. H. S.

NEWALA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu; baada ya

MSIMULIZI. 686

salamu, nakuarifu ya kwamba dunia yote ya Newala amani fi amani. June, mwezi thelitashara, aliwasili hapa Bwana Cook akitokea pande za Masasi; nlitoka hapana Bwana Askofu kwenda huko Masasi kutazamia watoto, naye kesha tazamia. June mwezi tissatashara ikawa shughuli ya kutazamia hapa petu, killa mtoto alijaribu kadiri yake. Aliyetokea wa kwanza katika I Class, 1 ni Adarou Saburi, 2 Eriko Akachigombo. II Class, 1 Nasro 2 Cecil Kansila III Class, 1 Kachinga, 2 Atanasio Sikela na Manji. IV Class, 1 Simani Mtopenyasa 2 Mmenyanga. V Class, 1 Liwasya, 2 Mikonga. Tuna darasa zapata nane lakini naona majina yatatosha.

June, mwezi asharini, Bwana Simpson alitoka hapa kwenda Masasi, kuwafanyizia Eukaristi Mt. alipokirudi akapitia njia za Chitangali kuwafanyizia na wao Eukaristi Mt. akarejea hapa July mwezi tatu.

Siku kuu ya Petro tukawa na furaha marudufu, kwani ndugu zetu wapata 60 wakapokea Eukaristi Mt. mara ya kwanza. Ilikuwa shughuli kubwa hawa wote kuwasharikisha mtu moja. Kwani Bwana Simpson alikwenda Masasi bassi akawa Bwana Smith peke yake. Tulipokwisha ibada hiyo tukafunga vyakula vyetu na masufuria tukashuka chini mahameni kwetu. Tukashinda huko kutwa, zilipotimia kama saa a thenashara unussu tukaanza kugeuza visogo kuja zetu. Tukarudi kwa mbalamwezi, watoto wakapendezewa mno, wakawa wakiimba tangu chini mpaka hapa. Siku moja, Juma a pili, ilitokea safari, itokayo pwani ya Mtamba. Safari kubwa sana ya Warungarunga, nao shidda kupita pande hizi. Safari hiyo wote wanena Kiswahili, nayo ni shidda watu wa barra wote kasema Kiswahili, Bassi hawa kisa cha kusema Kiswahili ni hiki:

Safari hiyo mkubwa wao ni Tereka. Bassi huyu

MSIMULIZI. 687

Tereka awali yake alitoka pwani ya Bagamoyo. Alikopa mali nyingi za watu akaenda pande za Tanganyika kutarathaki.

Alipofika huko washenzi wakataka kumpiga. Naye hakuwa peke yake alikuwa na watu wengi wa Mrima pamoja naye. Bassi watu wa inchi walipokuja akapigana nao akawashinda, hatta wakamtaka awe Sultani wao, naye akawaambia nakubali, lakini nataka kwanza mniletee masultani wenu wa kwanza niwaue; bassi nao wakaenda kuwakamata wakamletea akawaua, illa waliokuwa wakikaa mbali hakuwaua, lakini akawatiisha sana. Akawa yeye mfalme katika inchi hiyo. Na wale watu wa Mrima aliofuatana nao wakawatalaamisha watu wa asili hatta karibu wote wanajua Kiswahili.

Na huyu Tereka ushuru anaowatoza ndio killa atakapouawa tembo jino moja lake, Bassi kwa hivyo amekuwa tajiri sana. Hatta mwaka huu amekuja kupunguza pembe zingine. Amenunua nguo nyingi sana, na baruti. Tena amechukua mifuko mingi ya Rupia, na ginsi alivyozichukua nyingi unene huko pwani kuna mti wa Marupia aliokwenda kuchuma haya marupia. Na katika safari hiyo kuna mtu mmoja aliyekuwa akifundishwa dini ya Kimasihiya huko kwao, alipotaka kuniambia mafundisho yake aliokifundishwa juu ya kuumbwa ulimwengu, na maswali na majibu ya Katekisimo fupi, na amri kumi, lakini hakuweza kusema vema kwa Kiswahili, kwani huko kwao nao wanafundishwa kikwao.

Na mtu huyo ni marra ya pili kupita hapa marra ya kwanza alipita na Wadachi walipokienda juu ya Rovuma, kwani yeye alikuwa askari, hatimaye aliporudi Lindi akatoroka hatta akaangukia pande hizi. S. C.

MSIMULIZI. 688

MLIMA MLINGA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Na baada ya salamu nakuarifu habari kidogo za safari yetu, kutoka Unguja kufika Magila, sasa sikiliza, tumeacha Mbweni siku ya Juma a nne, May 9, tukalala mjini, hatta assubuhi wa Juma a tano tukaingia katika Stima ya Wadachi. Siku ile ile tukafika Tanga tukalala nyumba ya wageni, assubuhi wa Alhamisi, Siku ya Kupaa kwake Bwana wetu, tukawa njia ya Tanga. Siku ile ile tukafika Msalaka, tukafika tukalala pale, lakini wenyewe walikuwa hawako, walikwenda kutembea Pangani. Assubuhi wa Ijuma tukashika njia tukaingia Magila. Mwezi wa May tumepumzika, na tukitembea kidogo kutazama jamaa, walio karibu na Magila, bassi mwezi ukiisha, mnamo June 4, siku ya Juma a pili kwa saa nne unussu, tukashika safari kidogo, kwenda kutazama Misozwe, tukaingia jioni kabisa, na safari hii ndogo tulikuwa mimi na Dactari, na Miss Shaw, tukalala huko siku ya Juma a pili tukapumzika usiku ule.

Sasa yaja kusudi niliyonia kuandika habari za safari yetu, mimi na Miss Woodward, bassi assubuhi tukashika safari ile kubwa ya kupanda mlima, ulioabudiwa na washenzi zamani, na sasa pia, lakini si wengi wawaaminio kama zamani, mlima huo waitwa Mlinga na ukitazama wasema haupandiki, lakini wapandika Bwana, na watu walio mashujaa na hodari pia, bassi sikiliza nikuambie habari zake, watu wenyewe walikuwa 18 ndiyo mimi, Miss Shaw, Miss Woodward Maryamu wa huko Misozwe, sio Maryamu Swedi, lakini mwingine, na daktari, wangine siwezi kuwataja.

Bassi tukaanza kupigana na msitu, tukiingia katika msitu, msitu wa kweli, sio wa kuchezea, kwanza

MSIMULIZI. 689

tukiingia twathani mna nyama za hatari, lakini hatukuona nyama yoyote, illa msitu tu kama msitu aliouona. Mr. Stanley akisafiri: tukaeudelea hatta kufika mlimani juu juu sana, kweli kuliko yote, lakini neno moja tukifika mahali pa kupumzika mtu aliye kiongozi alinyang'anywa kofia yake na Sekiteke maana ya Sekiteke, ni baridi, bassi tukamwachia zawadi mkuu wa mlima.

Tukafika mpaka juu kama nilivyosema kwanza, na tukiishafika, baridi kali sana ilikuwako huko juu ukisimama katika kilele hicho, waona bahari ya Unguja, Pangani, na Tanga, killa mahali paonekana sawa, nayo ni inchi ya milima, lakini ukipanda huko yaonekana, kama hivyo nilivyosema, hatimaye tukarejea nyumbani kwetu hili neno la mwisho natumaini mtajua kama sisi wanne ni wanawake wa kwanza kufika Mlinga, na mimi mtoto wa kwanza wa Mission ya Mbweni niliyeuona Mlinga! kweli ndugu zangu, nilipouona na kuukanyaga nilikuwa kama wale Waargonauti waliosafiri kupata ngozi ya thahabu, kweli nilifurahi mno kufika huko Mlinga. Ndiyo mwisho. C. S.

KIUNGANI.

Kunako May 31 Juma atano tukawa na safari yetu kwenda Dunga kushinda huko badala ya Pentekote, kwani tungalienda siku zile zile za Pentekote, lakini kwa kuwa hatukuwa na buddi kumwendea kwanza General Mathews kwa kwenda huko na kukaribishwa na wasimamizi wale wa kule, bassi alipoulizwa yeye siku zile za Pentekote, akasema hawezi kwenda siku hizi kwani maji mengi njiani na mbu wengi huko, ngojeni kadiri ya siku nane ndipo mutaweza kwenda, lakini si huyo tu mimi mwenyewe nataka nipitie shambani

MSIMULIZI. 690

kwangu na kula chakula cha saa sita pale halafu ndio kwendelea. Bassi May 31 tukaamka hapa kama saa kumi tukafunga mizigo tayari kwa safari killa mtu akachukua mkeka wake, bassi tukaondoka hapa assubui na mapema kabisa tukashika njia ya kwenda Mwera, tukawa na mabwana wawili Mr King na Mr Ghambers.

Mr Chambers na Mwalimu Yohana Abdallah wakawa kiongozi wakawa mbele mbele, hatukupumzika mahali mpaka tulipoufikia mto Mwera tukapumzika, na hapa tukamkuta kijana kuja kutulaki, Auatoka wapi huyu? Ametumwa na msimamizi wa shamba lile la General Mathews kutuongoza mpaka hapo shambani, bassi hatukukaa sana pale Mwera tukaondoka kumfuata kijana huyu, tukaenda kama nussu saa tu tukawasili penyi nyumba zao, kweli ni mahali pazuri sana, tukakaribishwa barazani. Looo, baba, Msimamizi akaamrisha watumwa walioko kuangua madafu mengi sana sana, aliyekunywa mawili amekunywa aliyekunywa matatu amekunywa aliyekunywa manne pia hatta tukatoshewa madafu, tahamaki kidogo hivi twaona chakula kinaletwa tukala hatta tukashindwa. Kweli tukafanyiwa heshima sana tukajifurahisha hapa kama tulivyoweza wote.

Tukiisha kufaidi hapa hatukuwa na buddi kushika safari yetu kuendelea mbele kwani hatujafika mahali petu tunapokwenda, tukaondoka hapa pamoja na Msimamizi huyu kutusindikiza nussu njia akarudi, nasi tukazidi kuendelea tukafika Dunga saa tano, watu wa huko wakatukaribisha kama walivyoweza. Likini hawapiti wa hapa pa Muugwana. Zikatolewa fetha tukanunua mbuzi akachinjwa tukapika chakula tukala. Tulipokwisha killa mtu akajua kushika matembezi yake hatta jioni tukajipikia chakula chetu tukala, na kwa kulala Mr King akasema wapendao kulala juu ya jumba na waende na wapendao kulala

MSIMULIZI. 691

bandani ruhusa, bassi wangine wakalala juu na wangine wakalala humo bandani.

June kwanza ikawa shughuli ileile kutembea tu bassi na kula, Wangine wangalipenda sana kwenda kuangalia kinu wanapofanyiza asali ya miwa, asali nyingi sana inafanyizwa hapo tena ni asali nzuri sana inayofanyizwa hapa. June ileile kunako saa kumpitia na moja unussu tukashika njia kurudi kwetu, hatukuwa na buddi kumpitia na kumwaga Msimamizi yule wa Gen. Mathews. Mr Chambers na Mwalimu Yohana na watoto wangine walikwenda upesi bassi hawa hawakupitia kwa Msimamizi huyu wakapita kwa njia nyingine, lakini waliosalia nyuma pamoja na Mr King wakapita tukakuta makapo ya madafu chekwa tukayaingilia hatta tukayaacha waliokuwa na nguvu wakachukua wangine, tukaagana na Msimamizi huyu tukashika njia kukimbilia Mwera kusudi tuwapitie Mr Chambers na wangine, tukifika Mwera na giza yetu tukamkuta bwana Chambers yupo anapumzika na kutungojea sisi wa nyuma.

Tukatoka Mwera na giza kabisa tukafika hapa petu kama saa ya pili unusu ya usiku.

Kunako June 7, alisafiri mwalimu Yohana B. Abdallah kwenda Chitangali kukaa mahali pa Padre Cocil hatta arudipo, naye alifuatana na Archdeacon aliyekuwa akienda Dar-es-salama kuangalia mahali akaapo Padre Denys.

June 10, alifika Archdeacon kutoka Dar-es-salama, aliingia ndani ya chombo, alitoka Dar-es-salama saa a tano akafika bandarini saa thenashara June. 18, alituasilia mwalimu Lawrence Mmaka kutoka kuwatazama jamaa zake Bonde.

June 21, ilikuwa furaha sana kwani Bwana Askofu alituasilia hapa akitoka Newala, pamoja naye Padre Cecil

MSIMULIZI. 692

Majaliwa, na mwalimu Daudi Machina na watoto saba wa Newala; Isaya Mwalinjila, Cherubini Masaninga, Leslig Namate, Edward Suudi, Reuben Namalowe, Mika Twanje, Gayo Sifana, na watoto wawili wa Masasi Benedikto K. Njewa, Yona Makunda, na mwalimu Bernado Mpunga. Tena pamoja nao Kibwana Martini Y. Nakaam.

June 22, tulipewa nussu siku kucheza kwa heshima na kumkumbuka mwalimu Hugh S. Mtoka kwani amefanywa Msomaji huko Chitangali; na siku ya pili yake pia tukapewa siku nzima kwa ajili ya waalimu Samwil Chiponde na Sipriani H. Chitenje kwani wao pia wameamriwa kazi ya Usomaji.

July 13, tulifanya mashindano ya football sisi na Maofisari wa H. M. S. Raleigh, tulichezea pale kiwanjani petu; watoto wote wa Kiungani na Wazungu wetu, na Wazungu wengi wa mjini, watoto wa chuoni, na wa kazi wa Mkunazini pia pamoja na Wazungu wao walikuja kuangalia machezo; tulicheza sana. Sisi tulipata mabao sita kwa moja lao, tukaisha saa a thenashara. Lakini kushinda huku Wazungu hao wasikubali, wakasema watakuja tena siku ingine. July 16, Bwana Askofu aliwatia mikono watoto sita wa hapa, ndio hawa: Thoma Aundi, Daudi Kamanaa, S. Davis Kalinga, Luka Sitanili, Isaak Mayunga, na A. Henli Hasani.

July 18, palikuwa arusi Mbweni ya Padre Denys Sayite na Rabeka Wajionaje wote wa Kiungani tulienda billa wagonjwa tu, nayo ilistawi sana. Sala ilikuwa saa ya kwanza, tulipotoka kanisani tukapata chakula chetu cha assubuhi, na saa a sita waliokwitwa kwa arusi wakaenda kula kwenyi chuo cha watoto wa Mbweni, na wangine wakapewa chakula chao nje. Kunako saa a kumi unussu tukawa tunawapeleka bwana na bibi arusi nyumbani kwao, tukaenda kwa shangwi

na watoto wa kike wakiimba tu njiani mwote, na mwalimu W. E. Kanyopolea akapiga bunduki shibe yake. Hatta walipoingia nyumbani mwao wale waliowapeleka wakapakuliwa chakula kingi, saa ya jioni tukajirudia zetu.

July 19, alituasilia hapa mwalimu Herbert J. Sehiza akitoka Bonde kuangalia wazee wake kwa muda wa miezi miwili.

July 20, yalikuwa tena mashindano ya Wazungu wale wale wa H. M. S. Raleigh nao walisayidiwa na Balyozi Mr. Cave na Mr. Boustead, siku hii hatta watoto wa Mbweni walikuja kutazama, pamoja na Mr. Key & Miss Philips. Lakini kwa safari hii ya pili ilikuwa vita kubwa, tukapata mabao mawili kwa billa mwanda. Waliocheza walikuwa Klementi Mkajanguya mlangoni; Yohana Sonjo, Amini Mvuma, Backs; Julius Mkwaya, Cecil Majula, Frederick Makwela, Half-backs; Clement Kathibeni, Benedict Madalito, Right; Gray Feruzi, Centre; Danieli Usufu, Petro Sulemani Left; July 22, alifika mwalimu Elward Kingodi akitoka Bonde kuangalia jamaa. Hatta kwa siku hizi twatazamia mashindano tena na Wazungu kwani wamenena ya kwamba hawakubali, watakuja tena.

HABARI ZA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu, na baada ya salamu, habari zetu za siku hizi, ngoja kwanza nikuelezee. Panapo mwezi wa August 1 tulipata siku kuu ya kusafiri kwake Mwalimu Rebeka na mume wake, bassi wache hapo watoto wafurahie siku kuu lakini hatukwenda popote illa hapa petu. Tena panapo mwezi ule ule wa August 6 ilikuwa siku ya kuzaliwa kwake Askofu wetu, bassi siku yenyewe ilikuwa Juma a pili, naswi huku kusikia hivyo ilikuwa furaha tupu Mbweni, bassi taji zikafanywa haraka haraka tayari ya Juma a pili, ziende kwa Askofu wetu Kiungani, tulipokwisha kufanya zikaenda assubui mapema zikamfikia. Bassi hapo alipoziona mwenyewe, alifurahi sana, hatimaye jioni tukapata baina kama amezipata, akaamuru siku ya Juma a tatu tupate siku kuu, Mission zote, nasi siku

hiyo tulijikalia hapa petu, na saa tatu unussu tukaenda kujizungumza kidogo, na jioni kabisa tukarejea kwetu.

August 24, ilikuwa siku kuu ya Bartolomayo Mtume, siku hiyo ilikuwa mvua kufuru hatta mahali tulipotaka kwenda, hatukuwahi tukakaa hapa petu.

August 29, tulikwenda kushinda Kiungani, na huko tulifurahiwa sana, kwa sababu killa mwenyi mjoli wake akaonana naye na jioni tukarejea kwetu.

Sept. 8, Siku kuu ya Kuzaliwa kwake Bikira Maryamu, Kanisa jipya la nyumba ya watoto Mbweni ndipo tukalitabaruku.

Sala ya kwanza ikawa katika Kanisa la Yohana Mt.; Askofu akahubiri.

MSIMULIZI. 695

Siku yenyewe tukasimama mlangoni pa Kanisa jipya; Askofu na makasisi na waimbaji waliingia Kanisa dogo la zamani kusali; walipotoka wakaendelea hatta mlango wa Kanisa jipya: watoto wakasimama pande zote tangu mlango wa Kanisa la zamani mpaka mlango wa Kanisa la sasa. Waimbaji wa Kiungani walikuwapo wakisayidia waimbaji wa Kanisa la Yohana Mt. Mlango ulifungwa, Askofu alipofika mlangoni bassi tukaendelea tukazunguka nje ya Kanisa tukaimba Zaburi 51.

Tuliporudi ndipo mlango ukafunguliwa tukapata kuingia. Askofu aliomba sana; akalipa Kanisa hili jina la Bikira Maryamu Mbarikiwa: na Kanisa dogo limo ndani mwake amelipa jina la Mchungaji aliye mwema. Sala ya Kutabaruku Askofu alifanya Usharika Mtakatifu wengi walishariki.

Tulipotoka kanisani watoto wa Kiungani, na Mkunazini walifika maana walitangulia waimbaji tu walifika. Wamasihiya wote wa Mbweni waliojenga Kanisa walikuwapo Kanisani walipotoka wakacheza ngoma.

Tukaingia Kanisani tena athuuri tukaimba Litania, tulipotoka tukapata chakula. Saa nne u nussu Wazungu wengi wakaja kusali, Balyozi mkubwa na balyozi mdogo. Siku kuu ilisitawi sana. Sep. 9, Juma a mosi Askofu alitoa Usharika katika mathabahu ya kanisa dogo la Mchungaji Mwema. Watu wa Shamba wakacheza ngoma, wakapata karamu, Sep. 10, hatukutumia kanisa jipya illa kwa sala ya watoto wadogo.

Sep. 11 padre Key alitoa Usharika katika kanisa dogo la Mchungaji mwema.

Sep. 12, Askofu aliita watoto wote wa chama ya Mchungaji mwema na Watakatifu wote kwa chai. Akahubiri katika kanisa, akasoma amri ya Chama cha Watakatifu wote zilizobadilika. Akawaambia amri

MSIMULIZI. 696

zilizo bora za chama, ni kufanya kazi kwa Muungu na wagonjwa burre.

Akawaambia heri kutoka katika Chama wasipotaka kushika amri zile sana. Sep. 13, kulikuwa Usharika Mt. jioni watoto wote wa chuoni na nyumba ya kazi walicheza. Sep. 14, Usharika Mtakatifu katika Kanisa la Mchungaji mwema. Sep. 15, ndio Ocktavi ya sika kuu, watoto wote walienda kanisani tuliimba nyimbo zote vile vile kama siku ile ya kwanza. Hivi siku kuu imeisha. Imesitawi sana.

Sept. 21, ilikuwa siku kuu ya Mattayo, tulikwenda kushinda shamba la pili la Bibi Mwalimu kunako saa 9 unussu, hatta jioni tukarejea nyumbani.

Tena kunako Sept. 20, Padre Key, alifunga safari ya kwenda Dare-salama pamoja na mkewe; kutembea kama ilivyo desturi yake kuzunguka huko; hatta kwenyi Sept. 28 akarejea tena. Sept. 26, Ilikuwa harusi ya Constantine Mgoma na Lulu Masuke na Bernado Mpunga na Ethel Mzikapo na Andrea Andani na Edith Mary Kabutu. Tulikusanyika katika Kanisa la Bikira Maryamu Mt. karamu ilikuwa saa tano unussu, killa mgeni aliyekaribishwa kwa karamu hii akaja. Walikuwapo mezani wageni 102. Panapo saa kumi unussu bwana harusi na bibi harusi wakaondoka killa mtu kwenda nyumbani kwao. Constantine na Lulu wakaa shamba la Mbweni, na Andrea na Edith Mary pia wakaa shamba la Mbweni. Bernado na Ethel nyumba yao ilikuwa Kiungani tayari ya kungoja safari ya Newala. L. M.

HABARI ZA KICHELWE.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salamu.

Kuna watu labuda watakaopenda kusoma habari kidogo za safari yetu Dar-es-Salama. Tumeondoka sisi, ndio

MSIMULIZI. 697

Mr. na Mrs. Key na mtoto mmoja, mchana September 20 tukaingia Stima "Kaiser" tukafika karibu na Dar-es-Salama saa 12, lakini merikebu ikakwama tukaingia ghubba isizamishe dau ilioko njiani tukachelewa saa 2. Tukasayidiwa sana na Mbanyani jina lake Rattansay aliyefundishwa Kiunguja na Makasisi yetu Lindi na Unguja zamani sana. Huyu ni sasa mkuu wa forthani, tukaingia mashua yake tukafika pwani, tukakaa mjini usiku, tukamwandikia Mwalimu Denys atupelekee wapagazi. Tukawasalimia rafiki zetu mjini tukashika njia tukafika Kichelwe Alhamisi, tukapumzika kidogo njiani kwa mzee Kaungama, tulipomkuta Denys watu wengi wametulaki wametukaribisha vizuri, tukafika nyumba ya Mwalimu nzuri, imejengwa kilimani inaonekana mbali milima. Nyumba hii ina baraza kubwa nafasi kwa watu wengi wanaposali. Marra ya kwanza tumewahesabu waanake 51 na waanaume 38, killa siku 60 ao 70, Juma a pili watu 100. Tumefurahiwa kusikia kwa Shemasi Denys watu wengi huja killa siku kufundishwa assubui na jioni. Baada ya siku si nyingi natumaini watakuwa tayari kupokea msalaba. Ijumaa na Juma a pili tumekuwa na Usharika Mtakatifu baada ya Sala ya assubui. Jioni tukatembea mjini karibu tukakaribishwa po pote. Watu wengi walitaka dawa, sikuchukua illa kidogo tu, ni mahali baridi kuliko hapa, wengi walikuwa na kifua lakini waliotoka hapa wameonekana wenyi afya sana. Tumeona nyoka namna mbali mbali, mmoja chumbani mwetu, tukasikia fisi akilia lakini hapana wanyama wakali karibu, illa siafu na wadudu tele.

Juma a pili Padre na Mwalimu walikwenda mjini saa mchana kuwaswalisha watu wetu. Wakirudi tumesikia merikebu itawasili labuda jioni tuwe tayari kuondoka mapema Juma a tatu. Tukawafuata rafiki zetu wengi tukashika njia tukapita mjini saa pili. Mchana kutwa

tukangoja ile Reichstag isionekane, mwisho Bwana Mbanyani katuahidi tuondoke Juma a nne katika chombo cha forthani, tukalala nyumbani mwake. Tumeingia chomboni saa kwanza unussu tukatweka tanga tukaenda, tukaenda, tukajaribu kutoka bandari lakini tanga mbili, maji yakaanza kujaa sana tukachelewa hatta saa nane tungetumaini kuona Mbweni hatukuja pita pa kuingilia Dar-es-Salama, tukakata tamaa kufika Unguja, usiku tukaita ngalawa tukarudi mjini. Nicholas Faraji aliyesafiri Kilima-njaro akarudi siku hizi pamoja na askari, akanipa zawadi sungura mtoto aliyetoka huko, mzuri sana na mtulivu nikapendezwa sana naye, lakini hakuweza kuvumilia bahari ao chombo kafa siku ya pili. Hatukuwa na mahali pa kukaa askari po pote katika nyumba ya wageni, mwisho tukakaribishwa vizuri penyi Mission ya Wadachi tukapumzika. Nyumba ya wagonjwa pale pazuri sana. Juma a tano saa kumi Stima Reichstag ikawasili tukaingia usiku tukaonana na Mr. Hainsworth. Assubui mapema tukaondoka tukatia nanga Unguja saa 4 tukafurahia safari yetu na kurudi pia. E. K.

HABARI ZA CHITANGALI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salama. Hatuna mengi kuwaambieni, kama nitumainivyo mtazidi kuniwia rathi maana nasema mlioisha jua wengi wenu.

June 16 tumeanza kujenga nyumba hapa, msimamizi ni Mwalimu Hugh Mtoka, lakini sasa isipokuwa bado kupigiliwa chini nayo ni kubwa sana kwa kadri.

June 22 watu wa Masasi na wa Newala walipita hapa kutoka Lindi wamechukua mzigo, Mwalimu Yehana akawamo katika safari hii, watu walifurahi mno kumwona wakacheza ngoma jioni kwa kumfurahia mno; na mamaye akatoa zawadi nyingi kwa watu, waliocheza ngoma.

MSIMULIZI. 699

Kunako siku hizi palikuwa na uthia mwingi wa kusema kama Madachi wanamwendea Machemba kumpiga. Bassi Machemba asema nyakati nitakazoshindwa na Mdachi, sitakubali kutawaliwa nao lakini nitakimbia kwa njia ya Mwenye Barnaba Nakaam. Bassi wetu wote wa hapa na Wamakonde walikuwa tayari wampige kwa selaha, maana yee Machemba hangepita kwa amani hapa, alisema atapita kwa vita. Kwa siku zote asema, Mzee Nakam ndiye anayenichongea kwa Madachi wanipige, maana yee amepatana nao. Bassi watu wangine ndio hawa watu wa Mitema na watu wa Manyamba walipatana na Machemba kwa shauri hilo kuja kupiga mji huu wa mzee Nakaam, bass walipoona vita ya Madachi hapana, June 23 wakaleta watu wengi wao kuja kuomba msamaha wakisema kama hawakufanya shauri hilo, Mwenye B. Nakaam amewasamehe. June 28, Mwalimu Yohana alienda Makonde kuwahubiria.

June 30, Padre Simpson na Mr. Hunter walituwasilia hapa, Mr Hunter alimpeleka padre maana yee padre ni adui sana na jua; bassi akawa anamtunza njiani, asiugue. Lakini Mr. Hunter assubuhi akarudi Masasi.

July 1, Mr Cook akaja hapa toka Newala, kwa kusudi awatazamie watoto wetu elimu (Examination).

July 4, Mr. Cook akarudi Newala kwa njia ya Miwa anakokaa mwalimu Yustino Mkandu, ussubui watoto wa chuoni walipata siku kuu kucheza kupumzika kwa "Examination" yao.

July 10, mwalimu Yohana alienda kutembea Newala na Miwa hatta Masasi, akarudia hatta hapa, akatumia siku nane.

July 20, nilienda Masasi nikatumia siku nane kwenda na kurudi, wakati wa kurudi nimekuwapo na Mr. Hunter amekuja hapa kupunga hewa kidogo maana ameshughulika mno kule Masasi, Padre Porter alipokuwa Unguja.

MSIMULIZI. 700

Lakini akashinda siku moja: na subui akaenda Newala kumwona Padre Carnon. Juma apili saa 8 usiku akarudi pamoja na Mr. Cook. Naye Mr. Cook anashuka zake Unguja maana thaifu anaenda kupata shauri kwa mganga wa kubadili hewa.

Bwana Smith amekuwapo hapa juzi kwa kusudi la kutufanyia Usharika Mt: sasa amekwenda zake Masasi kwenda kufunga mizigo, maana anashuka zake Unguja kwa safari yake ya kwenda Nyasa.

July 29, imewasili safari hapa ya watu wa Makanjila wamechukua pembe nyingi nao wengi sana, wakashinda siku mbili, sasa wameenda zao Lindi wamewatoroka watumwa wao watatu hatta sasa hawaonekani waliko. A.K.

HABARI ZA KIUNGANI.

Habari zetu za safari hii ni chache nazo ndizo hizi:

Aug. 1, watoto wa Classes zetu mbili walicheza ndio 1 na 2 Class, walicheza kupumzishwa kidogo kwani kunako July 27 & 28 walitazamiwa akili. Tena siku ile ile jioni yake Mwalimu Denys na mkewe aliingia melini kwenda Dare-salama, pamoja nao waliingia mwalimu P. H. Musa na Barnaba Mtaula na Y. M. Nakaam waliokuwa wakienda zao Chitangali, meli yao ikaondoka Aug. 2.

Aug. 5, tulimsafirisha ndugu yetu Yohana Sonjo kwenda Uganda, kusudi awapikie Wazungu wapelekwa waliokuwa wanakwenda huko, kwani yeye ni mpishi.

Aug. 6, Ilikuwa kuzaliwa kwa Bwana Askofu, lakini hatukuweza kujifurahisha sana kwa kuwa ilikuwa Juma apili, lakini Juma atatu Aug. 7 watoto wote wa Kiungani tulienda kisiwa Bawe kushinda huko pamoja na Mr.

MSIMULIZI. 701

King, na watoto Choir school Mkunazini pamoja na Dr. Palmer, siku hiyo tulifurahiwa sana, wakati wa kwenda wangine waliingia katika mashua ya moshi wangine katika mashua tatu zilizofungashwa. Kisiwani kule, tulipofika tu ilikuwa killa mtu kwa njia yake, wale waliokwenda kuwinda wakamkamata paa mzima wakamleta tulipotulia, lakini baadaye kwa kumchezea-chezea wakamtorosha. Saa asita tukapata chakula chetu. Baada ya kula, wangine wakaenda kuchezacheza tu, na wangine wakachukua mashua kuzunguka kisiwa chenyewe. Saa ya jioni tukarudi kwa taabu ya mawimbi, tukafika hapa Kiungani karibu na saa apili.

Aug. 8, Eredrick Makwela aliingia katika kufanya kazi ya dobi. Aug. 10, tulishindana tena na Wazungu wale wale tukashinda pia. Aug. 10, waliingizwa waalimu wangine, ndio Petro Sulimani, Karlo E. Lisomba, Elvani Kachawa, Paul Dezu, Yohana Hamisi, Gabriel Katoma na Silwano Ngaweje.

Aug. 14 na 15, darasa zetu mbili zingine zalifanya Examination, ndio darasa ya tatu na ya nne. Walioshinda ndio hawa, Class 1, 1 Daniel Usufu, 2 Klement Mkajanguya, 3 Cecil Majula. 2 Class 1 Paul Dezu, 2 Gabriel Katoma, 3 Class 1 Bemado Mkaki 2 Y. W. Akupata. 4 Classi 1 Alfred Mlisho, 2 Brnno Sauli.

Aug. 24, ndio siku kuu ya Bartolomayo tulienda Mkunazini kwa sala ya Usharika Mt: kwa ginsi ya shangwi, naye Bwana Askofu alikuwapo. Tena siku ile ile walituasilia mwalimu Constantine Mgoma, W. J. Swedi na Tomaso Yanikore wakitoka Magila. Aug. 28, tulipamba nyumba yetu, Aug. 29, ikawa mkutano hapa watoto wa Mbweni, wa Mkunazini na sisi, tulifurahi sana siku hiyo, jioni killa mtu akarudi kwake. Aug. 30, Luka Sitanili alienda kukaa Mkunazini anajifunza kazi ya kufua fetha.

MSIMULIZI. 702

Sep. 1, mwalimu Antonio Misimile alisafiri kwao Zaramo akipitia njia ya Bagamoyo, alienda kuangalia jamaa yake, alikaa siku mbili tu, akafika tena bapa Sep. 4, siku ile ile akapata chombo kwenda Magila kufundisha. Tena siku hii hii Sep. 5, watoto wawili Thoma Aundi, ha Aidan Mekenda waliingia kazini ya kupiga chapa.

Sep. 22, Ilikuwa siku ya chama ukawa Usharika kwa watu wa chama assubuhi, tena saa atatu yakawa mahubiri kwa darasa ya kwanza na ya pili wapendao.

Sep. 28, alitufikia Mr. Hainsworth naye alipita kwa Cape. Na siku ile ile Tomaso Yanikore aliingia kazi ya upishi.

Sep. 29, ilikuwa safari ya Mr. Hainsworth, na Bernado Mpunga na mkewe, na watoto wawili waendao kwa wazee wao ndio Silwano Ngaweje na Yusuf Kasembe, wamekwenda Newala, tena siku hii hii Mr. King alifunga safari ya kwenda Bombay kwa nduguye, na baadaye aende zake Ulaya.

Oct. 1, Tumeangukiwa na msiba wa ghafula, ndugu yetu mmoja Daudi Kamanaa, baada ya kuugua kwa siku moja, panapo saa sita ugonjwa ukamzidi; marra akaenda kuitwa mganga, akaja kumtazama. Hatta saa tissa Muungu amependa kuitwaa roho yake katika ulimwengu huu wa taabu. R.I.P. Mtg.

HABARI ZA MKUNAZINI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu, illi wa baada ya salamu sikiliza habari nikupe, tazama katika Msimulizi wa 30, ukurasa wa 680 utaona kama palikuja habari za vita ya pande wa juu, bassi sikia nikumalizie: Hao wenyi maprende wakaenenda pamoja na askari zao, wakafika. Ee bwana, naye mshenzi ya macho, walimkuta, kwani

MSIMULIZI. 703

aliwavurumisha hawa wacheza gwaride mpaka killa mtu akatafuta njia kwa meno asione, hatta akina General Matthews wakapanguliwa tepe zao za begani kwa risasi, illi sababu na tena sababu manuari moja ya Mwingreza illi kuwa pamoja nao, bassi wale wana maji wa Kizungu ndio waliotenda shughuli kweli kweli, kwa bombom zao na mizinga ya kukokota waliwavurumisha washenzi sawa sawa; lakini hatta hivyo Wazungu wawili watatu walijeruhi, weusi pia walikufa, na wangine kujeruhi, lakini wameipata inchi hiyo; General Matthews na Hatch wamerudi, pamoja; na askari nussu, wangine wamesalia kuulinda mji na kuzidi kulishana chuma na hawo washenzi. Amepelekwa Kaptain wake kuwa mkuu wa hapo mjini palipotwaliwa. Ndio habari za kule tumo katika kusikiliza tu kwani watu wangine kawajarejea.

Siku ya Aug. 2, pamepita hapa Shemasi Denys pamoja mkewe wakienenda Dar-es-Salaam kukaa huko, kwani wameisha jenga nyumba yao, mbali kidogo na mjini kama toka Kiungani hatta Mbweni shambani pande hizo na mahali penyewe paitwa "Kichelwe?"

Panapo siku ya Aug. 4, alasiri ametuasilia ndugu yetu Charles W. Rehani, aliyesafiri pamoja na Askofu Tucker kwenda Uganda, bassi sasa amerudi naye. Lakini Askofu sasa kaenda zake Ulaya na Charles akaa Mbweni na mkewe, mpaka wapatapo safari ya kurejea Uganda. Siku ya saba ya Aug. watoto wetu walipata siku kuu wakaenenda Bawe pamoja na watoto wa Kiungani kwa kufurahia siku kuzaliwa kwake Bwana Askofu.

Panapo Aug. 16 ametuasilia Padre Smith akitoka pande za Yao Newala, akifuatana naye Mr. Cook ajaye kupunga hewa baada ya ugonjwa mzito wa siku nyingi, tena Hugli S. Mtoka, & Sipriani Chitenji waendao Kiungani kuzidi kusoma kwani waalimu.

MSIMULIZI. 704

Siku ya 21 watoto wetu watatu tumewapeleka Kiungani, kwani wamepata cheo cha kutosha cha kukaa Kiungani, nao ni hawa, Tustino Dodo, Marko Mradi na Victor Magonga. Siku hii baba yake George Uledi kafariki, yule aliyekuwa mwashi jina lake Yohana Uledi mumewe Margaret Maharamno akaaye Ngarabo.

Panapo siku kuu ya Bartolomayo hatukwenda pahala illa tumeshinda papa hapa tu.

Panapo siku ya Sept. 6 Joseph Chabwela kapata mtoto mwingine mwanamke, panapo Sept. 8 Frank E. Dema kapata mtoto naye mwanamke.

Panapo 14 siku ya Msalaba Mt. watoto wa Mr. Lister, ndio ya nyumba ya kazi walienda Dunda tulipanda punda wote tulifika huko tukashinda usiku mmoja tukarudi zetu siku ya Ijumaa alasiri kasiri, siku kuu ile ilifayidika kwa upande wake.

Panapo 17, wamebatizwa watoto wawili wa yule Joseph jina lake ni Eva, na yule wa Frank Dema jina lake ni Fidea Mary.

Siku hizi hizi pametufikia bibi wawili wakitoka Ulaya Ingreza, kazi yao ni katika Hospital majina yao ni Miss Saunders na Miss Willion wakaa Hospital.

Panapo siku hiyo hiyo pametufikia wageni wa Ulaya Ingreza, wamekuja pamoja na Mr. Joseph Williams aendaye tena Nyasa, akichukua pamoja naye Padre Glossop na daktari Robinson wote waenda Nyasa. Waliokaa Unguja Mr. Hitchborn akaaye Kiungani kazi yake mwalimu, na Mr. Brockway amerejea tena pande za Magila yeye huyu alipotoka Ingereza tu, alishuka pande za Tanga kwani aliingia katika meli ya Wadoicha.

Tena wakumbuka kama Seyid alikuwa na simba wawili, dume na jike, sasa hapana, wale simba amempelekea Bibi Queen huko Ulaya Ingreza kuwa zawadi yake. Na

MSIMULIZI. 705

mahali pale palipokuwa tundu lao hao simba, sasa pamejengwa kibanda kidogo cha bati kwa askari wakeshao pale kuwekea mavazi yao.

Juzi juzi Charles W. R. kapata barua za Uganda, na na moja yatoka kwa yule Henry Wright Duta, akimwandikia hivi - "Mpenzi ndugu, Siku ile ile mlipofika upande wa pili wa Nyanza kutoka Mengo ndio siku ya themintashara ya mwezi June huku nyuma ikaanguka vita ya nguvu sana, vita hiyo ni ya Waislamu, hao Waislamu walifanya shauri na wale askari wa balyozi wa kule, Wanubi Manjolinjoli, wakawaambia, nyie njolinjoli kwa nini kumtumikia Mzungu nanyi ni Waislamu? Wao wakasema sisi twatumika kwa mshahara si burre, lakini wale Waislam wakawaambia njolinjoli, tazama, fanyeni hivi, njooni nyie nyote tuunganike pamoja tuwe jeshi moja mwasini Mzungu, mje tufanye vita kubwa na hawa Wazungu pamoja na Waganda wote walio Wamasihiya, akiwa Mfransa ao Mwengreza haithuru tuwapige tu, na tukiwashinda inchi iwe yetu; njolinjoli akakubali shauri, wakapatana siku ndio siku ya Juma a pili wakiingia kanisani kusali, twende tukawachinje kama kuku tu. Wakasema vema Juma a pili kazi. Bassi, kumbe kwa bahati habari zikafika kwa Wamasihiya, wale Wamasihiya wakaenda wakampasha habari balyozi na mkuu wa askari, Bassi Captain Arthur akapiga torumpeta, akawakusanya askari wote, wakaja, akawapiga forin. Akawaambia, nataka askari wote waache bunduki bandani wasitembee nazo kama kawaida, hivyo tu, bassi wote toka njolinjoli hatta nani wakaziweka bunduki bandani na viasi vyake pia wakatoka wakaenda zao.

Haya bassi Juma a pili ikaja, hapana mtu aliyeenda Kanisani, illa chache, kwani wote walijiweka tayari kumbe kweli vita ikatokea, marra ngoma ya vita ikapigwa. Ah!

vita kali nje Mzungu akawagawia Wamasihiya wangine bunduki vita ikasaki sawa sawa, hatta watu wengi walijeruhi na kuuawa, lakini Waarabu wakashindwa, wao na njolinjoli zao, wakafukuzwa weee hatta inchi ya Unyoro, majeshi ya Waganda mangine yakarudi ya kasalia mangine yakizidi kuwafuata tu. Kwani ni furaha sana kwao kuwaondoa hao Waislamu bassi wamewafuatia habari hazijaja bado; ndio habari. W.E.K.

HABARI ZA MASASI.

Twawaarifu habari chache za hapa, siku hizi tumo katika furaha ya Siku kuu ya Bartolomayo Mtume. Kwanza siku yenyewe Aug: 24 assubui kama saa a pili ikapigwa kengele ya Eukaristi Mtakatifu. Baadaye kama saa a tatu u nussu yakawa mashindano ya watoto na watu wazima, kwa kukimbia mbio, na kuruka, na kutupa jiwe, na bunduki na kuvutana kamba.

Michezo ilipokwisha tukaenda mezani kula chakula cha aththuuri.

Labuda wangine wameisha sikia kama mahali hapa nyumba za Mission wanahamisha kujenga upande wa pili wa mlima huu Mtandi; bassi jambo la kwanza ni kujenga Kanisa mbele ya kujenga nyumba zingine. Na Kanisa hilo litajengwa na Wamasihiya na Waanafunzi, burre billa mshahara, na msingi ukawekwa katika Siku kuu ile ya Bartolomayo panapo kama saa kumi u nussu. Nalisahau kusema kama katika Siku kuu ile Aug. 24 ya Bartolomayo Mtume, mbele ya kuanza Sala ya Eukaristi Mtakatifu walipewa msalaba jumla watu 20, kufanywa Waanafunzi.

Waalimu wawili wapo hapa kwa siku kuu hii - Arthur na Yustino pamoja na watoto wao wa Mlolela ha Miwa. Nao wanarudi kwao Sept: 1, tayari kwa kufungua

MSIMULIZI. 707

vyuo vyao Sept. 4, Watoto wa hapa nussu wamekwenda Newala na nussu wapo papa hapa. Salamu! Y.M.

MKUZI.

August 1, walituasilia hapa Tomaso Yanikore na wenzake wakitoka Unguja.

Aug. 5, alituasilia baba J. E. Griffin akitoka Kologwe.

Aug. 16, walifika hapa waalimu wawili ndio Constantine Mgoma na Cyprian Lizani, na mtoto Tomaso Yanikore pamoja na George Kanakwao wakitoka Magila, na C, Lizani akitoka pande za Misozwe.

Aug. 18, waalimu wale wakatuacha, C. Lizani amekwenda zake Misozwe, na C. Mgoma amekwenenda Msaraka kuamkia watu. Assubui yake siku ile ile akatufikia Padre Smith akitoka Unguja.

Aug. 21, waalimu hawa Willie J. Swedi na C. Mgoma wamesafiri kwenda zao Unguja pamoja na watoto wawili Tomaso Yanikore na George Kanakwao. Nimesahau Aug. 20, ulikuwa ubatizo wa mtoto wa Henry Nasibu. Salaamu. W. M.

HABARI ZA KIUNGANI.

Safari hii naja na habari kidogo tu. Oct. 2, mwalimu Paul Dezu amesafiri kwenda kwao Bonde kutazama jamaa zake.

Oct. 6, ametuasilia mtoto mmoja wa Mkunazini jina lake Boniface Toro kuja kukaa hapa.

Oct. 12, Ametuasilia mwalimu Yohana B. Abdallah akitokea Chitangali pamoja naye mwalimu Petro H. Musa, na Barnaba Mtaula, na mtu mmoja Adamu Twanje amekuja kuuguzwa mkono.

Oct, 15, tumefurahi mno sisi watu wa chama maana jamaa yetu imerudi, ndio mwalimu Yohana Hamisi ameingia "Chama cha Paolo Mtume."

Oct. 16 na 17, Waalimu walitazamiwa akili zao (Examination).

Oct. 25, tumemsafirisha Mwalimu Klementi Mkajanguya kwenda Masasi aanze kazi yake ya kufundisha, alifuatana na watoto watatu wa

Chitangali waendao kutazama jamaa zao; nao ni mwalimu Daniel Usufu, Karlo Edward Lisomba, na Gilbert Y. Mpalila.

Nov. 7, tuliitwa Mbweni kwa harusi ya mwalimu Leonard Mkwasomba na Charlotte Mary M., na Yohana Nibakali na Olive N., hatta jioni mwalimu Leonard tukamleta mpaka hapa Kiungani ndio masikani yake, na Yohana Nibakali tukamsindikiza mpaka Mkunazini ndiko iliko masikani yake.

Nov. 14, Bwana Askofu amewasili Unguja akitokea pande za Bonde.

Nov. 17, Alban Njengune amerudi Unguja, maana kwa miaka mitatu alikuwa Mombei akifanya kazi ndani ya Manoari moja ya Kiingreza.

MSIMULIZI. 709

Nov. 19, tumefurahi mno, maana Bwana Gillanders ameturudia tena, maana yeye ni mwalimu wetu, alikuwa hawezi sana, bassi doktari akaonelea heri asafiri baharini mpaka Natal kwa mwezi mmoja, bassi akasafiri; sasa amepata afya amerudi. Nov. 22, Bwana Askofu amesafiri kwenda Newala pamoja na Mr. Cook anaenda kuwa mwalimu wa watoto, tena amefuatana na mwalimu Kolumba Y. Mzigala anaenda kutazama jamaa zake na baada ya mwezi atarejea tena. Siku ile ile usiku waalimu wa Kiungani waliitwa Mbweni kutazama mchezo wa Kekilia Bikira Mtakatifu, Ah! ulitupendeza mno.

Nov. 26, imekuja meli ya Nyasa na Mzungu mmoja Bwana Crouch, wamefuatana naye watoto kumi wa Kinyasa wajao kusoma hapa, majina yao ni haya; Mwalimu Mikael Chikokota, na watoto Leonard Mattiya Kamungo, W. Hilary Likwambe, Ciprian F. Kaule, Edward F. Konganya, Frederick M. Taweni, Herbert M. Mwarabu, George W. Mwenyeze, Barnaba L. Mnena, na Allen Mwachibi. Tumefurahi mno kuwapata.

Nov. 25, zikatangazwa habari ya kuwa watakaribishwa watu wa zamani waliokaa chini ya dari ya nyumba ya Kiungani ya Andrea Mtume, bassi kwanza wakachaguliwa wakubwa watano Robert Feruzi, Owen Makanyasa, Michael Gudula, Heath Darueshi na mwalimu William Edward Kanyopolea; wakapewa karatasi ndogo zenyi jina ndani yake zimepigwa chapa, bassi hawa wakazitawanya zile karatasi kwa killa mmoja aitwae karamuni, wakapatikana watu settini na tatu waliokaribishwa.

Nov. 30, Siku kuu ya Andrea Mtume na Sh. Assubui saa kwanza ilikuwa sala kubwa ya Usharika, halafu tukatoka kanisani. Marra wakaja wapishi wawili na mbuzi mmoja, wakamchinja, wakamtengeneza, bassi wakaupika wali wa pilao, hatta wakaisha. Tena yakaja makombe

MSIMULIZI. 710

thenashara na vikombe 60 vya chai, marra ilipopata saa tatu unussu ikapigwa kengele, tukapamba uani na chuoni na mezani kwa bendera tupu.

Tulipokwisha kupamba tukawa watu wa kupumzika tu, lakini kufumba na kufumbua ikawa jioni, ilipotimu saa thenashara wageni walioitwa wakatuasili tukafurahi kuonana nao. Chakula kikaanza kutengenezwa tayari, marra hiyo kengele zikapigwa, watu wakaingia kanisani, na kanisa likajaa watu. Sala ya jioni ikaanza kwa shangwi sana, halafu Archdeacon Jones-Bateman akatoa khutuba juu ya maneno "Isa Masiya jana na leo yuleyule, na hatta milete."

"Labda nyie watu wa zamani, mnaona kanisa na pambo lake ni lingine limebadilika, tena Ah! Kiungani imebadilika siyo kama zamani; na watoto wote wageni. Tena Wazungu wageni, akina Bishop Tozer na Bishep Steere na Bwana Randolph hawapo, hakosi mnasema, Ah! siye atujuaye nani? Sisi sasa hatuna mchunga. Lakini yuko mmoja asiyebadilika, yupo mmoja asiyepita, yuko mmoja tu awachungaye. Tazama wangine mmesafiri mbali hatta kuzunguka Afrika yote, na wangine mpaka Kongo na Kepi, lakini yule Mchungaji mwema aliwafuateni na kuwalinda salama katika safari zenu, Isa Masiya jana na leo yuleyule, na hatta milele."

Bassi khutuba lilipokwisha, tukamaliza sala zetu za jioni kwa shangwi waimbaji tukizunguka ndani ya kanisa tukiimba; halafu sala zikaisha.

Tulipotoka ndipo wageni walioitwa wakaingia karamuni, killa mmoja akatoshewa kwa furaha. Walipotoka mezani ndipo ikaanza michezo uani tukacheza wangine askari na wangine tinge. Hatta ilipohitimu saa tatu unussu ikapigwa kengele, wote tukaenda chuoni kwa "Kwimbato," tukaimba na watu wote waliokuwapo wakapendezwa mno, hatta saa nne kassorobo "Kwimbato" ikaisha. Tukaagana

MSIMULIZI. 711

kwa furaha na wageni wetu, tukawaacha wakaenda zao, ndivyo tulivyofurahi kwa siku kuu ya Andrea Mume na Sh., tunakusudia tufanye vile vile siku ingine tukijaliwa.

Dec. 3, mwalimu Benedict Madalito amesafiri ndani ya jahazi ya Kinuguja kwenda Dare-salaam, amekwenda kukaa kwa siku chache Kichelwe mahali anapokaa Padre Denys Sayite, kupunga hewa. Mtg.

MKUNAZINI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi wasalaam. Illi wa baada ya salaamu, illi sikia mtathaa wa barra hii; Unirathie kwani nalisahau habari kidogo katika mwezi ule, ndio panapo Sep. 3, Ndugu yetu Willie W. Boga alifariki kule Hospital.

Siku ya 23, pametuasilia Bwana Hainsworth akitoka Ulaya Amerika, illi kusudi kurejea katika shughuli yake, pamoja naye Padre J. K. Key na mkewe akitoka Dar-es-Salaam illi kumwangalia Mwalimu Denys na shughuli yake, Sep. 29, pametupitia Bwana Hainsworth na Bernado Mponga na mkewe wakisafiri kwenenda barra Newala. Sep. 30 Mke wa Barnabas Farijallah kapata mtoto mume. Oct. 12, Twaliona moto pande za mchangani, Ah! moto huu ulibatili vitu kathawakatha, hatta roho za watu pia nyingi zalibatilika, lakini, mwenyi kuchoma moto alikamatwa, alivyotendewa ni vile vile vya killa siu, ameuawa. Siku hiyo hiyo pametuasilia mwalimu Yohana A. Abdallah, Paul Kasese, Petro Musa, na Barnaba Mtaula, wakitoka barra Newala illi kwenda Kiungani.

Panapo Oct. 15, Mtoto wa Julia Farijallah kabatizwa jina lake Mikael Steere King. Mnamo Oct. 24, pametufikia Bwana Atlay akitoka barra Nyasa, akienenda Ulaya Ingreza kupunga hewa. Oct. 31, Ilikuwa sala ya

MSIMULIZI. 712

shangwi sana katika Christ Church, kwa kuwa mbela ya siku yu Watakatifu; na Nov. 1, ilikuwa sala kubwa na shangwi pia. Tena, mchana, Bibi Boyd na Daktari na Mr. H. Faulkner &c. walikaribisha watoto wa Mkunazini, lakini walio Kiungani, na wangine watu wa Mgongo-Ngamia, na watoto wa Sagara, ndio watoto wa kazi wa Mr. H. Lister, wakawaita rafiki na wale wenyi mama wakaita mama zao kuja kula karamu ya siku kuu ya Watakatifu wote. Mnamo saa ya alasiri wakaagana wakaenenda zao. Panapo siku hiyo hiyo tumepata habari ya Miss Shaw kafariki, ilikuwa huzuni sana kwetu sisi. Wajua kama panapo mwezi February Balyozi mkubwa wa hapa Unguja alitumwa illi kuenenda Uganda, bassi akaenenda kakaa sana huko hatta mwezi huu wa juzi akarejea tena hapa, wallakini wapi bwana, hakukaa sana hapa, marra ilikuja simu vile vile ya kuwa aenende. Bassi hayupo hapa, illa wapo wangine tu.

Panapo Nov. 2, Ametuasilia Padre Denys S. na mkewe wakitoka Mrima Dar-es-saalam.

Nov. 6, Tumepatikana na ajali, ndio mtoto wa Frank E. Dema amefariki ghafula alikuwa mgonjwa wa kifua.

Nov. 7, huko Mbweni kulikuwa harusi bassi bwana harusi mmoja kaja kukaa hapa Mkunazini ndiyo Yohana Nibakali na mkewe ni Olive binti Uledi nduguye Nicholas Kusi. Lakini kazi yake hufanya kule kule Kiinua Mguu ndio ya Chapa.

Juzi juzi nimepata habari, ndio hizi jahazi bwana, lalipakia watumwa ishara yake likatweka bandera ya Kidoicha likitoka pande za Mrima, hilo jahazi likaja zake hatta ras-KisimKazi likatua likatia nanga, haya bassi likaanza kupakua. Walakini kwa ajali tu, palikuwa na watu wawili huko pwani wavuvi wakaangalia mambo yale yatendekavyo kwa haraka, napo ni usiku, bassi wakajua thabiti kama ni watumwa wale, nao wale

MSIMULIZI. 713

ni haba sana, hawakuweza kuwastusha. Illa walikiangalia sana chombo na ginsi watu wanavyopakuliwa na kuendeshwa haraka haraka kabisa. Bassi wakashika njia wakaja zao mjini wakapasha habari, marra Stima katta ya H. M. S. Racoon yalikwenenda mbio mbio, wakalikuta jahazi, haina watu, wakatafuta wenyeji wakaonekana, nahotha, na Waarabu wangine. Haya bassi shauri, Watumwa wapi? Ah! bwana, watumwa hapana, vema wale Wazungu wakafanya hila yao, ndio wakawatwaa wakulimani wakavalia kama mtu fullani tu, wakakaa huko pwani wale wenyeji wasipojua kama ni waviziaji wametumwa na serkali ya Ingreza. Bassi, Ah! bwana hayakukawia, marra waliwagundua watwana wajinga wakawasairi sana sana, hatta mambo yote yakawa wazi wazi, wakapatikana watu kama watu 33 ao zayidi ndio mhabari. Hili ndilo shauri la siku hizi kama mtu ye yote ajapo akaona jahazi ao ngalawa ao mtumbwi umepakia watumwa, akaja akanena kwa wakuu wa Unguja atapata thawabu yake kubwa, na heshima yake.

Tena amri imetoka, jahazi lolote lile halina ruksa kutweka bandera yoyote ile, illa mpaka iwe ya rayia yake, killa tntu afanye ya rayia yake, kusudi mambo yasichafuke. Tena amri ingine, jahazi likiisha tweka na kupewa Cheti ya safari na kuamriwa muda wake wa kutoka, bassi halina ruksa tena kutia nanga popote katika kisiwa cha Unguja illa kipate ruksa kule kule forthani. Hatta juzi juzi jahazi moja limekamatwa; laliisha pakia, likapewa ruksa likatoka, likaja zake hatta ras Mbweni likatia nanga, marra ghafula, Stim katta hiyo jahazi likatiwa mkononi. Shauri, mbona hivi? Ah! ah! bwana mtu mmoja kaenda pwani kuleta mafenesi, Wakaambiwa, Iko wapi cheti ya ruksa? Ah! hatuna. Bassi njooni, wakarudishwa wale manahotha wakatiwa gerezani. Bassi waona amri kubwa siku hizi Unguja, yote hayo yawe imara.

MSIMULIZI. 714

Tena siku hizi killa nyumba yatoa ushuru na killa nyumba yatiwa nambari, killa nyumba kwa kadiri yake kwa kadiri ya nyumba ilivyo, ndivyo hutoa.

Nov. 14, Askofu karejea akitoka barra Shambala.

Nov. 17, pametuasilia Bibi C. Thackery akitoka Ulaya Ingreza pamoja naye Keziah Shikalako na Bibi Breay mkuu wa Hospitali hii.

Siku iliyofuata tumepata watoto watano wakitoka kwa Balyozi, wawili wako katika chuo cha Miss Mills na watatu kwa Mr. H. Lister.

Wale wawili majina yao ni Kapanga na Idi, na wale watatu ni, Kanyenda, Matola, na Chiungamangoma, wote kwa jumla ni Wanyasa illa mmoja ni Mngoni; huyu Kapanga ni mtumwa wa Pemba, penyi mji Kasugulu, na huyu Idi atoka pa Mponda yule yule wa Nyasa. Kanyenda atoka Nkota-nkota kwa Jumbe, Mangoma kwa Mhalule na Matola kwa Chitambe inchi ya Wayao; ndio habari zao. Nov. 22, Askofu kang'oa nanga akienenda barra Newala, pamoja naye Padre Denys S. na mkewe wakirudi zao Mrima Dares-Salaam.

Nov. 24, Meli ya Ulaya iling'oa ikichukua Mabibi wetu wawili na mwalimu Hilda Siyenu afanyaye kazi Hospital kuwa msayidia wa hao, wanaenenda hapa Mombasa kupunga hewa kwani walipatikana na ugonjwa sana.

Tumefurahi kumwona Padre wetu Tyrwhitt akitoka pande za chini kwani alikwenenda kupunga hewa baada ya ugonjwa wa siku nyingi, pamoja naye Mr. Gillander wa Kiungani. Lakini naona hakukumfaa sana kwani kule chini waliwekwa katika mji mmoja kwa siku nyingi (Quaranteen) kwani merikebu yao ilitoka katika inchi ya homa.

Naona mtafurahi kusikia kama panapo Juma a nne Christopher Kiwapo amemwoa Ellen Fayida wa Mbweni ndio habari.

MSIMULIZI. 715

Hapa niandikapo tu katuasilia Bwana Crouch atokaye Lake Nyasa, pamoja naye mwalimu Mikaeli Chikokota na Leonard Kamungo na watoto wangine nane — wote wamekuja illi kutafuta elimu hapo Kiungani. W. E. K.

HABARI ZA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Baada ya salaamu nakuarifu habari hizi haba na chache, natumaini kama utakuwa rathi kwayo.

Nov. 7, ilikuwa harusi ya mwalimu Leonard Mkwasomba na Charlotte Mary Kabutu, Yohana Nibakali na Olive Uledi, ilikuwa harusi nzuri, wageni wengi walikuwapo mezani.

Nov. 7, Kurudi kwa Bibi yetu Miss Thackeray na ndugu yetu Keziah Shikalako, watokao pande za Ulaya Ingereza. Tumefurahi sana kuwaona wakirudi salama salamini, Miss R. Barkeley aliposikia kama wamekwisha fika katika bandari ya Unguja alifunga safari ya kwenda kuwalaki. Sisi watoto alituamuru kutengeneza nyumba, mnamo saa kenda naswi pia tukatoka kukutana nao, tukakutana nao karibu ya Kiungani. Si furaha hiyo kuonana nao tena!

Nov. 21, Tukapata siku nzima ya kucheza tulipata kwa ajili ya kurudi bibi Miss Thackeray, jioni tukaenda katika shamba lake, killa mtoto akapata ndizi, mnamo saa edashara unnsu tukarejea nyumbani maana saa karibu kwenda Kanisani.

Twafurahi kwamba yeye bibi anaonekana yu hajambo kidogo.

Nov. 3, Ilikuwa kusanyiko la Chama ya Mchungaji Mwema, siku ileile mtu mmoja akaingia ndiye mwalimu Nina Madisa.

Nov. 28, ilikuwa arusi ya Christopher Kiwapo na

MSIMULIZI. 716

Ellen Fayida, nao wakaa mjini, hii ni arusi ya tatu iliyoozwa katika kanisa letu hili la Maryamu Bikira Mtakatifu.

Nov. 80, Siku kuu ya Andrea Mt. tulifurahi mno kwayo, Padre Dale akatutolea Usharika Mt. maana Padre Key alikwenda pande za mrima Dar-es-salaam.

Dec. 1, Kusanyiko la Chama ya Mchunga Mwema, siku hiyo hiyo mtu mmoja akaingia ndiye mwalimu Clara Kabutu, sisi watu wa Chama hiki twafurahi kwamba twaongezeka zayidi, Padre Dale alituhubiria vizuri sana juu ya Chama chetu. K. Sh.

HABARI ZA SHAMBA LA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi, I11 jenab, salaam. Nathani utapenda kusikia habari kidogo za huku, kwa muda wa miezi hii haba niliyokaa tangu kuoa.

Habari zenyewe si nyingi, labuda miezi ijayo. Kwanza juu yangu mwenyewe kama nilianza kazi ya kufundisha watoto wa huku shamba, katika mwanzo wa Oct. ya mwaka huu. Sasa watoto wote waliokuwa wakisoma Kiungani wa Shamba hili, sasa wapo hapa wanasoma. Nami nina watoto 28, ndio habari zangu.

Sasa zingine za huzuni! Twasikitika sana kama katika mwezi mmoja tumepatwa na huzuni tatu.

Katika Oct. 1, ndugu yetu mmoja Agnes Kaiwale aliitwa na Muungu kutoka katika dunia hii ya thambi. R. I. P.

Katika Oct. 11, walitokea usika watu wasafiri watano walimtaka Padre awapatie pa kukaa naye akawapatia. Kushinda siku mbili, alitokea mtoro mmoja kwa ujanja kutaka hati ya jahazi na kusafiri salama, bali Padre alijua, akamjibu kama nenda mjini, marra assubuhi yake, bwana zake wakawasili kwa kumtafuta. Wakapewa ruksa kumtafuta popote ndani ya shamba hili.

MSIMULIZI. 717

Oct. 12, ndugu mwingine aliitwa na Muungu; Musa Njala aliugua siku nyingi sana. R.I.P.

Oct. 18, siku kuu ya Luka, hatukuenda popote. Oct. 22, Eva Kawazi alipata mwana, bali usiku huo huo alifariki. Na Oct. 25, ilikuwa harusi kati ya Matola na Brauch Mdachimwa.

Oct. 30, Lydia Mwarabu alipata mtoto mke.

Nov. 2, Usiku saa ya pili alituwasilia mwalimu Denys na mkewe kutoka Dare-salama.

Nov. 12 ilikuwa ubatizo wa mtoto wa Ruppert Mwarabu na jina lake aitwa Emily Mary Patience.

Nov. 17, aliwasili Alban Njengune kuteka Bombay. Nov. 21, mwalimu Denys na mkewe walifunga safari ya kurejea kwao Dare-salama. Ndiyo habari. C. M.

NEWALA.

Kwa muda mwingi sijashika kalamu vyandani mwangu kukuarifu habari za Mrima huu wa Newala.

Mwezi tissa, October, watu wote walifurahi kumwona Padre Harnsworth tena, aliyetoka kwa muda wa mwaka hapa. Watoto wengi pamoja na Padre Carnon tukaenda kumkuta kwa Naliogo, kama mwendo wa saa tatu tangu hapa, tukachukua na vyakula vyetu, na maji, kwani mnajua inchi ya Makonde haina maji. Bassi tulipofika tukamkuta ameisha wasili kwa Naliogo. Bassi tukakaa pale kupumzika na kupika vyakula vyetu hatta saa a saba tulipokwisha tukaja zetu. Kuwasili tu mjini tukaanza kupiga vigelegele, na bunduki, wakazidi kufurahi kumwona Bernado na mkewe. Na mwezi sitashara ilikuwa arusi ya watu wawili, Austini Asmani na Augustino Somaili.

Nov. Mwezi mosi, siku kuu ya Watakatifu watoto wa nyumbani tulishuka chini mahameni, kwenda kutengeneza pahala pa kufanyizia Eukaristi Mt. penyi kiwanja cha

makaburi, kwani keshoye ni siku ya Roho zote.

Bassi alfajiri nikaondoka niwe pamoja na watoto watatu, na vijana wawili waliochukua vyombo, na mavazi ya wakati wa Eukaristi Mt. tena mathbahu ndogo ya marhemu askofu Mackenzie tukachukua kwenda kufanyizia Eukaristi. Bassi vile vyombo nilivyotanguliza nikaweka tayari na mavazi, hatima akaja Padre pamoja na watu. Akaanza kufanyiza Eukaristi, tena akahubiri kidogo, kuwaeleza sababu ya kushuka chini, na alipomaliza Eukaristi tukafunga vyombo vyetu kuja zetu.

Tuna habari ya huzuni iliotupata mwezi huu, ndio kufa kwake Yakobo Akumtemba babuye Bernado, alifariki mwezi thelitashara alfajiri kama saa edashara, na papo assubuhi ukafanyika Eukaristi kwa ajili yake, na mshuko wa alasiri tukaenda chini kumzika. R. I. P. S.C.

HABARI ZA CHITANGALI.

Habari zetu ni chache na thaifu, maana mkewe Mikael Hamisi alizaa mtoto, na yule mtoto amekufa, tena baada ya siku tatu Mama naye akafariki; naye ni mwanafunzi. Tena mtoto wa Adamu Twanje amefariki: Kwa habari ingine ndio, Wamasihiya wengi na waanafunzi wamehama kwenda kukaa Mwiti, kama mwendo wa saa tissa kutoka Chitangali mpaka Mwiti, bassi ni taabu kwao kuja kusali hapa, hatta wangine wanapoa moto wao wa kumtumikia Muungu, maana wanakaa mbali na kanisa lao. Katika mwezi wa November, panapo athuuri marra tukaona moshi mwingi mji wa Msokosela, kutahamaki tukaona nyumba zinaungua moto. Watu wakajaribu kuuzuia wasiweze, maana manyasi ni kama baruti kwa moto; bali kwa rehema ya Muumba wetu zikaungua nyumba nane tu, na katika nyumba hizo hapana kitu kilichookoka. Tumefurahi mno kumwona Bwana Askofu

MSIMULIZI. 719

na watu walishangilia sana, tena watoto walioenda Unguja kusoma wamerudi hapa kutazama jamaa zao, ndio mwalimu Daniel Usufu, Carlo Edward Lisomba na Gilbert Y. Mpalila, lakini walitoka hapa kwenda Newala kutembea, na wakapita Masadi kumtazama Padre Carnon, na wakarejea kwa njia ya Mwiti, na kufika hapa.

Padre ameona vema Mikael Hamisi arudi kukaa Mission, maana ya kupatikana na msiba mkubwa. Wutoto wetu waume wanaendelea sasa katika kusoma, na watoto waanawake wamefurahi mno kwa kumpata mwalimu Rose Muriezai kuwafundisha chuoni: balli amekuja kutembea tu, na baada ya miezi miwili atarudi Unguja. Mwenye Barnaba Nakaam alienda kuwinda mwezi wa November, alipata nyama 68, amezikamata kwa wavu, tena siku hizi watu wanafanya kazi ya kulima. Tena Mzee Machemba bin Mchakama, ameleta wajumbe kwa Mwenye Barnaba Nakaam na Mzee Matola wadi Mbuzi, kusema kama ataka apatane nao, waende kwake wafanye mapatanishi. Balli mzee Barnaba Nakaam na mzee Matola, killa mmoja amepeleka watu wawili wawili kwenda kwa Machemba, kupata habari hiyo ya amani; balli mzee Machemba amewarudisha wale watu wanne, kusema kama mapatano haya hataki yafanyike na wadogo, illa aondoke mzee B. Nakaam na mzee Matola waende kwa mzee Machemba, wapatane wao kwa wao, lakini bado kwisha, nitawaarifuni ginsi yatakavyoishia. Mtg.

HABARI ZA NYASA.

Salaamu sana kwa Mtengenezaji wa Msimulizi, na baada ya salamu, nakuarifu habari kidogo. Furaha gani tuliyo nayo sisi kwa kumpata Baba wa rohoni! Kwani Baba wa zamani sasa ni mzee hangeweza kutembea tena huko na huko; kwa rehema ya Muungu amewezesha kufanya

MSIMULIZI. 720

mashauri kututafutia Askofu mpya. Huyu Askofu, Blantyre alimtia mikono Mzungu mmoja wa Company. Tena alipofika kwenyi milki yake akawa na kazi kubwa sana ya kuzungukazunguka huko na huko kutia mikono kwa killa kijiji, kwani Wamasihiya wengi walikuwa bado kutiwa mikono; na akawatia zayidi ya watu arobaini, (Akasema; leo nimekuwa na furaha kwa sababu nimewatia mikono watu wengi). Kwa sisi bin adamu twamwona ni wema na mpole natumaini kama miaka ijayo watu watazidi sana kumgeukia Muungu, akizidi kuishi. Naye hupenda kutembea pande zote, akafika Blantyre mpaka Zombe illa pande za kaskazini hajafika bado kwani ataka sana kupatana na watu na kujua hali yao walivyo. Tena siku hizi wamefanya mashauri kufanya Mission mbili. Archdeaeon Maples Mission yake ndiyo ya Unangu pande za Wayao, na Rev. Johnson pande za pwani toka Ngofi mpaka Mponda. Panapo mwezi wa September, Archdeacon Maples na Doctor Hine na Reginald wakashika safari ya kwenda Unangu na watu hamsini waliofuatana nao, nayo ilikawa Juma a tatu. Archdeacon akarudi Alhamisi na wale watu hamsini, akasalia Doctor Hine na mwalimu Reginald Songolo, kufundisha na watoto wawili wa kumsayidia na mpishi mmoja Simeon K. Mjeleka. Habari za Doctor Hine kaenda kama kujitoa sadaka hatujui kama huyo Kalanje kakubali kwa moyo mmoja ao sivyo, (Kalanje ndiye mfalme wa Unangu). Na kama ataka kupatana na Wazungu kuikubali Anjili kwa moyo nionavyo na nitumainivyo kwa rehema za Muungu itazidi kuendelea mpaka tutakuwa Mission moja na pande za Newala na Masasi baadaye. Rev. Johnson anaanza sasa kujenga nyumba kwa Mponda kaenda mwalimu mmoja William Y. Kang'oma na watoto wangine kumsayidia, kiisha atarudia tena Utonga, kwani ndiye mwalimu wa Utonga. Nimesikia kama waalimu watakuwa wakienda mwezi kwa mwezi kufundisha huko

MSIMULIZI. 721

kwa Mponda. Tena steamer za Balyozi Johnstone mbili zimeisha na ya Wissman moja. Tulipofika Pinda tukasikia kwa simu kama Makanjila kaisha fukuzwa naye kakimbilia milimani na wamejenga ngome naona itakuwa amani tupu, kwani ndiye aliyekuwa akifanya uthia sana.

Tena jambo moja tunalotumainia sana na la furaha kusikia kama mwalimu Augustine Ambali anakusudiwa kupewa daraja takatifu ya Shemasi itakuwa furaha kubwa sana kusikia kama kaisha tiwa, hatujui ni siku gani, (na tuzidi kumwomba mkuu wa mavuno apeleke watu wengi katika mavuno yake). Kwani tutumainilo kwa rehema za Muungu kuondokesha wengi katika watu weusi kwa kazi ya Kanisa lake.